SUPA JACKPOT
TZS.1,109,975,029
KWA TZS. 1000 TU!
SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!
SportPesa.CO.TZ
PIGA *150*87#



**Bangi** mithili ya sigara yanaswa katika kiti cha dereva wa basi

UKURASA 3




UKURASA 11

Alhamisi Mei 4, 2023 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

# Nipashe

ISSN 0856 • Na. 0581300
www.ippmedia.com
MWANGA WA JAMII
The Guardian digital nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710
LIKE & FOLLOW US



# JIMBONI KWA SPIKA

• **Tulia** awasilisha hoja kuligawa, Sugu afunguka... *Endelea ukurasa 2*

## YALIYOMO

UKURASA WA 3
**ZUIO UVUVI ZIWA TANGANYIKA LAZUA MJADALA BUNGENI**
UAMUZI wa serikali za Tanzania, Burundi, Zambia na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (DRC) kufunga shughuli za uvuvi katika Ziwa Tanganyika, umezua...

UKURASA WA 4
**CRDB YAPATA LESENI YA KAMPUNI TANZU DRC**
BENKI Kuu ya Congo (BCC) imeipatia leseni ya kufungua kampuni tanzu nchini humu Benki ya CRDB...

UKURASA WA 5
**PROFESA JAY AJITOKEZA, ASHUKURU CCM, CHADEMA**
ALIYEKUWA Mbunge wa Mikumi, Joseph Haule, maarufu Profesa Jay, amejitokeza kwa mara ya kwanza baada ya kuugua kwa takribani mwaka mmoja na kuwashu-




Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, akizungumza katika maadhimisho ya miaka 30 ya Siku ya Uhuru wa Vyombo vya Habari Duniani Kitaifa Mkoa wa Mjini Magharibi jana. **PICHA: IKULU**

## Kambaya akimbia CHADEMA siku 53 kisa ubunge

UKURASA 7



## Wadau waja na maazimio 30 uhuru vyombo vya habari

UKURASA 2

MICHEZO NABI AWAONYA YANGA KWA MARUMO UK.24 KATUNI UK.6



Rais Samia Suluhu Hassan, akiongoza kikao cha Baraza la Mawaziri Ikulu Chamwino mkoani Dodoma jana. **PICHA: IKULU**

# Wadau waja na maazimio 30 uhuru wa vyombo vya habari

**Na Mwandishi Wetu**

WANAHABARI na wadau wa habari nchini, wametoa maazimio 30 kuboresha, kutetea na kulinda uhuru wa kujieleza na vyombo vya habari ambayo ni mambo ya msingi katika kukuza na kuimarisha haki za binadamu.

Maazimio hayo yalitolewa jana wakati wa maadhimisho ya miaka 30 ya Siku ya Uhuru wa Vyombo vya Habari Duniani.

Mwenyekiti wa Chama cha Waandishi wa Habari Wanawake Tanzania (TAMWA), Joyce Shebe, alisoma maazimio hayo katika kilele cha maadhimisho hayo yaliyofungwa na Rais wa Zanzibar, Dk. Hussen Ali Mwinyi. Kaulimbiu katika maadhimisho hayo ilikuwa 'Kuunda Mustakabali wa Haki, Uhuru wa Kujieleza Kama Kichocheo cha Haki Zingine za Binadamu'.

Kwa mashirika ya habari na wadau, alisema yanapaswa kuwakutanisha waandishi, wabunge wanawake na wanafunzi wa kike ili kujadili ukatili wa kimtandao na kuwajengea uwezo wa kutumia mitandao kwa ajili ya utetezi.

Pia alisema lengo ni kufanya upembuzi wa miradi ya mafunzo kwa waandishi na kuainisha upungufu ili kutumia rasilimali kwa usawa, kuendesha na kufadhili mafunzo ya kidigitali, mabadiliko ya tabianchi, uchafuzi wa mazingira kwa waandishi wa habari ili kuwajengea uwezo kuhusu masuala hayo.

Azimio lingine ni kutetea na kulinda maslahi ya nchi katika kukuza uhuru wa vyombo vya habari na haki za binadamu kuliko kutanguliza maslahi ya wafadhili.

Wadau na mashirika, pia alisema watoe ufadhili wa rasilimali fedha na teknolojia ili kuwezesha uendeshaji wa madawati ya jinsia katika vyombo vya habari na kuhimiza ushiriki wa wamiliki wa vyombo vya habari katika midahalo na jitihada mbalimbali za kutatua changamoto za waandishi wa habari.

**VYOMBO VYA HABARI**

Shebe alitaja maazimio kwa vyombo vya habari kuwa ni kuweka utaratibu wa kurithisha ujuzi na uzoefu kuendeleza vipaji

vya waandishi wa habari chipukizi watakaoleta mawazo, fikra mpya

na ujuzi wa kidijitali vitakavyochochea ubunifu katika vyumba vya habari pasipo kukiuka maadili ya uandishi wa habari.

Jukumu lingine alisema ni kuboresha mazingira ya kazi kwa waandishi wa habari ikiwamo kuwapo kwa mikataba ya ajira; kutoa mishahara kwa wakati na kutoa bima ya afya. Pia kuendesha mafunzo ya mara kwa mara kwa waandishi wa habari,

wahariri, wazalishaji na mameneja wakuu ili kuongeza mnyororo wa thamani katika utoaji wa maudhui sahihi, masoko na biashara.

Azimio lingine ni kuwekeza kwenye teknolojia ya kidijitali, ubunifu na kutumia mifumo mbalimbali ya kibiashara ili kuongeza mapato kupitia kuzalisha maudhui yenye ubora na yanayolenga mahitaji ya watumiaji.

**WAANDISHI WA HABARI**

Shebe alisema waliazimia kuwa waandishi wa habari waripoti taarifa za maeneo ya pembezoni na kupaza sauti za wasio

na sauti ili kutatua changamoto za kijamii na kiuchumi.

Pia alisema waandishi wa habari watumie nafasi zao kupaza sauti za wanawake

na makundi maalum wakiwamo watu wenye ulemavu na wanaoishi

kwenye mazingira magumu na hatarishi. Pia waandishi wajenge mazoea na utamaduni wa kujisomea na kuwa wabunifu kupitia kujifunza stadi mpya za kidijitali ili kuendana na kasi ya mabadiliko ya sasa duniani.

Alisema pia waandishi wa habari wanawake watumia fursa za kidijitali kujiendeleza kiujuzi na kiuchumi, kutangaza kazi zao na mafanikio huku wakizingatia usalama wao watumiapo mitandao ya kijamii.

Shebe alisema vyuo na taasisi za mafunzo zimetakiwa kujumuisha masuala ya ulinzi na usalama wa waandishi na kozi ya

matumizi ya kidigiti katika mitaala ya mafunzo kwa waandishi wa habari.

**SERIKALI**

Shebe alisema azimio la wanahabari kwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ni kuona namna ya kuharakisha mchakato wa Marekebisho ya Sheria ya Habari ili kuwezesha wanataaluma wa habari wa Tanzania Visiwani kupata sheria hiyo.

Alisema pia serikali ya Muungano iangalie namna ya ufuatiliaji wa kina wa vyombo vya habari vilivyosajiliwa ili kuhakikisha vinalipa kwa wakati mishahara na stahiki zingine za waandishi wa habari.

Pia alisema serikali ione umuhimu wa kuharakisha mchakato wa marekebisho

ya Sera ya Habari na Utangazaji ya mwaka 2003 ili iendane na muktadha na mazingira ya sasa.

TCRA katika maazimio hayo, imeshauriwa kuongeza jitihada za ufuatiliaji wa maudhui kwenye mitandao ya

kijamii hususan inayodhalilisha utu na heshima na kuhamasisha vitendo visivyo vya kimaadili katika jamii.

**MWINYI ASIFU UHURU**

RAIS wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, amesema wimbi la vyombo vya habari Tanzania limechangia uhuru wa kujieleza na kutoa habari huku akibainisha kuwa serikali zote mbili zinathamini uhuru wa habari na mchango wake katika maendeleo ya nchi.

Akizungumza katika kilele cha maadhimisho hayo, alisema taarifa kutoka Idara ya Habari (Maelezo) Tanzania Bara zinaonyesha kuwapo kwa magazeti 312 yaliyosajiliwa nchini hadi Februari 20, mwaka huu, wakati baada ya Uhuru wa Tanganyika, kulikuwa na magazeti 10.

Pia alisema kwa mujibu wa Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) hadi Februari, redio 218, televisheni 68, redio za kimtandao nane, Televisheni za mtandao 391, blog na majukwaa 73 vimesajiliwa Tanzania Bara. Tofauti na hali hiyo, alisema baada ya uhuru kulikuwa na kituo kimoja cha redio cha Tanganyika na hakukuwa na kituo cha televisheni, blogs wala majukwaa ya mtandaoni.

"Kwa upande wa Zanzibar, vile vile kumekuwa na kasi kubwa ya usajili mpya wa vyombo vya habari hasa vya kielektroniki kupitia Tume ya Utangazaji. Takwimu za tume hiyo zinaonyesha kuwa TV 21 za kawaida na 38 za mitandaoni zimesajiliwa. Aidha, radio 27 zikiwamo za masafa ya FM na za jamii zimesajiliwa," alisema.

Dk. Mwinyi alisema kwa mujibu wa Tume ya Utangazaji Zanzibar ongezeko kubwa la usajili wa vyombo vya habari limeonekana zaidi kati ya mwaka 2020 hadi 2023 na kwamba kuongezeka kwa idadi hiyo kumechangiwa zaidi na kukua kwa teknolojia ya habari na mawasiliano.

Alisema katika kufanikisha utoaji wa habari kwa umma kupitia mitandao ya kijamii, aliipongeza serikali ya Muungano kwa kufanya marekebisho ya kanuni za utangazaji na kupunguza tozo zilizokuwa zinalipwa na watoa huduma za mitandao ya maudhui nchini zikiwamo blogs, redio za mtandaoni na televisheni za mtandaoni.

"Hatua hizo zilizochukuliwa na serikali zinalenga kukuza dhana ya uhuru wa vyombo vya habari na kutanua wigo wa utoaji na usambazaji wa habari nchini. Hii ni kuonesha dhamira njema ya serikali katika kupanua uhuru wa vyombo vya habari ambazo ni miongoni mwa haki zinazotambuliwa katika Katiba zetu,"alisema.

**IMEANDALIWA na Rahma Suleiman, Mary Geofrey (ZANZIBAR) na Romana Mallya (DAR)**

# Spika wa Bunge awasilisha hoja kuligawa jimbo

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

WABUNGE akiwamo Spika wa Bunge, Dk. Tulia Ackson, wamewasilisha maombi ya kugawa majimbo yao kutokana na ukubwa na wingi wa watu.

Naibu Waziri Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Uratibu na Bunge, Ummy Nderiananga, alibainisha hayo jana bungeni alipojibu swali la nyongeza la Mbunge wa Viti Maalum, Sophia Mwakagenda.

Katika swali lake, mbunge huyo alisema Jimbo la Mbeya Mjini ni kubwa na lina kata 36 na kuhoji lini litagawanywa ili kurahisisha namna ya kulitumikia jimbo hilo.

Akijibu swali hilo, Nderiananga alisema mbunge wa jimbo hilo ambaye ni Spika wa Bunge, ameshawasilisha ombi na lipo mezani na muda utakapofika Tume ya Taifa ya Uchaguzi itaangalia.

Mbunge wa Kishapu (CCM), Boniphace Butondo, alisema jimbo lake lina kata 26 na kuhoji mkakati wa serikali wa kuhakikisha linagawanywa.

Katika swali la msingi, Mbunge wa Kilindi (CCM), Omari Kigua, alihoji lini serikali italigawa Jimbo la Kilindi.

Akiuliza swali la nyongeza, mbunge huyo alihoji mkakati wa serikali kuhakikisha maeneo madogo ya kiutawala hayapewi mgawanyo wa rasilimali sawa na maeneo makubwa kiutawala.

Akijibu maswali hayo, Nderiananga alisema wa sasa Tume ya Taifa ya Uchaguzi ipo katika maandalizi ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2025.

"Hivyo, kwa kuzingatia taratibu na vigezo, muda wa kugawa majimbo utakapofika tume itatoa tangazo rasmi kwa wadau wote wa uchaguzi juu ya kuanza kwa mchakato wa ugawaji wa majimbo ili wadau wawasilishe maoni na maombi yao na hivyo kushughulikiwa kwa mujibu wa vigezo vilivyowekwa kikatiba," alisema.

Aliongeza kuwa serikali inatambua kuwapo maeneo makubwa na madogo ya kiutawala na itahakikisha wananchi wanafikishiwa huduma stahiki.

Aliwahakikishia wabunge kuwa maombi waliyowasilisha yatafanyiwa kazi kwa kuangalia vigezo husika na kuomba watoe maoni na ushirikiano.

**SUGU ALONGA**

Alipotafutwa na Nipashe kuzungumzia hoja hiyo, aliyekuwa Mbunge wa Mbeya Mjini (CHADEMA), Joseph Mbilinyi, maarufu Sugu, alisema alikuwa safarini na alikuwa hajapata taarifa hiyo.

Alipoulizwa ikitokea jimbo hilo likagawanywa kama ana mpango wowote wa kugombea na atafanya hivyo upande upi, Sugu alijibu kwa kifupi "suala la jimbo kugawanywa na kugombea havina uhusiano. Niache nipo kwenye kikao."

HABARI KITAIFA



Mfanyakazi wa kujitolea kutoka Taasisi ya Time to Help Netherland, Reyham Yoldirim (kushoto), akishirikiana na wenzake kukata utepe kuzindua jengo la watoto yatima walilolikarabati kwa Sh. milioni 57 katika kituo cha Hiari cha Kingugi Mbagala, mkoani Dar es Salaam jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Zuio uvuvi Ziwa Tanganyika lazua mjadala mkali bungeni

**Na Gwamaka Alipipi,**
DODOMA

UAMUZI wa serikali za Tanzania, Burundi, Zambia na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (DRC) kufunga shughuli za uvuvi katika Ziwa Tanganyika, umezua mjadala bungeni baada ya wabunge wanaotoka mikoa inayopitiwa na ziwa hilo kuitaka serikali kusitisha uamuzi huo.

Mwezi uliopita mawaziri husika wa nchi hizo waliingia Mkataba wa Makubaliano (MoU) wa kufunga shughuli za uvuvi ndani ya Ziwa Tanganyika kwa muda wa miezi mitatu kuanzia Mei 15 hadi Agosti mwaka huu ili kuongeza idadi ya samaki.

Bungeni jana, wabunge wanaotoka mikoa ya Kigoma, Katavi na Rukwa, wakati wakichangia makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa mwaka ujao wa fedha, waliitaka serikali kusitisha mpango wa kuzuia uvuvi katika ziwa hilo, wakisema utaathiri uchumi wa wananchi wa mikoa hiyo.

Mbunge wa Nkasi Kaskazini (CHADEMA), Aida Khenani, alisema serikali inapaswa kutoa tamko kuhusu suala hilo kwa sababu macho na masikio ya wananchi wanaopitiwa na ziwa hilo yako bungeni, wanataka kujua hatma yao endapo litafungwa.

Alisema ziwa hilo kwa upande wa DRC sehemu wanayolitumia ni asilimia 45, Tanzania asilimia 41 na asilimia zingine ni za nchi zilizobakia ambazo ni Burundi na Zambia.

Aida alisema Ziwa Tanganyika ndiyo uchumi wa mikoa ya Kigoma, Rukwa na Katavi kama ilivyo kwa wananchi wa Lindi na Mtwara ambao wanategemea korosho.

"Hii miezi mitatu iliyotolewa serikali imewafikiriaje wananchi? Kama sababu ni kupungua kwa samaki siyo Ziwa Tangayika tu bali maziwa yote.

"Serikali inapaswa itafute njia mbadala kwa sababu kila samaki wakipungua itakuwa inafunga shughuli za uvuvi, mimi ninashauri vitengenezwe vizimba vya samaki ili kutatua tatizo hili pamoja na kupambana kutokomeza shughuli za uvuvi haramu," alisema.

Mbunge wa Kigoma Mjini (CCM), Kilumbe Ng'enda, alisema serikali inapaswa kusitisha mkakati huo. Iwashirikishe wananchi katika kufungwa kwa ziwa hilo.

"Wananchi wengi wanategemea Ziwa Tanganyika kupata kipato. Sasa likifungwa wataishi vipi? Tuna taarifa kwamba Tanzania tumefunga lakini wenzetu wa DRC bado hawajafunga," alisema.

Ni hoja iliyomlazimu Mbunge wa Kawe (CCM), Josephat Gwajima kusimama na kuomba kutoa taarifa, akisema "Serikali iangalie kama ni kweli wenzetu wamefunga, itakuwa ujinga sisi tufunge halafu wenzetu waendelea."

Mbunge wa Kigoma Kusini (CCM), Nashon Bidyanguze, alisema: "Ninaunga mkono hoja, serikali iangalie upya, sisi watu wa Kigoma tunategemea uvuvi. Serikali iwashirikishe wananchi ili wapewe mawazo mbadala. Wananchi wameniambia wengine wamenitumia ujumbe wa simu kwamba niwatafutie kazi pindi ziwa litakapofungwa."

Mbunge wa Viti Maalum (CCM), Sylvia Sigula alisema zimebaki siku nane shughuli za uvuvi katika Ziwa Tanganyika zisitishwe lakini idadi kubwa ya wananchi hawajashirikishwa katika mchakato huo.

Sigula alisema: "Ninaongea kwa niaba ya wabunge wa mikoa inayopitiwa na ziwa hili (Tanganyika). Tunataka serikali isitishe tamko hilo hadi pale itakapokuja na njia mbadala ya kuwasaidia wananchi kiuchumi".

**WAZIRI AFAFANUA**

Akitoa ufafanuzi kuhusu suala hilo kwa waandishi wa habari nje ya Ukumbi wa Bunge jana mchana, Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Abdallah Ulega aliwatoa hofu wananchi wanaoguswa na ziwa hilo, akieleza serikali inatafuta namna bora ya kutekeleza suala hilo itakayokuwa na manufaa kwa wote. Ulega alisema watakutana na wakuu wa mikoa yote mitatu, wabunge, wakuu wa wilaya, madiwani, wananchi na wakurugenzi kuzungumzia kwa kina suala hilo.

Ulega alisema" "Hii ni kwa sababu hata hawa wabunge siyo kwamba hawataki ziwa lifungwe, bali walilalamikia kutoshirikishwa kwa wadau wote. Mimi na wenzangu tunalichukulia jambo hili kwa umakini mkubwa. Tunaomba wananchi wasiwe na wasiwasi na taharuki, waendelee kufanya kazi zao kwa amani pasi na shaka yoyote."

Alisema itifaki inaruhusu nchi wanachama kufikiria namna bora inayoweza kufuatwa kuitekeleza.

"Sisi kama Watanzania tutafikiria pamoja njia bora ya kutekeleza hili kwa namna bora itakayofaa kwa wote. Hakuna haja ya taharuki," alisisitiza Waziri Ulega.

# Mabunda 50 ya bangi mfano wa sigara yanaswa Tunduma

**Na Moses Ng'wat,**
SONGWE

JESHI la Polisi Mkoa wa Songwe limekamata mabunda 50 ya sigara ambayo ni paketi 500, yenye uzito wa kilo nane, ambazo zimetengenezwa kwa kutumia bangi zilizokuwa zikisafirishwa kutoka Zimbabwe kuingia Tanzania.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Songwe, Kamishna Msaidizi (ACP) Theopista Mallya, alithibitisha kukamatwa kwa dawa hizo za kulevya na kuwaeleza waandishi wa habari kuwa zilikamatwa Aprili 29, mwaka huu, majira ya saa 2:45 katika mpaka wa Tunduma.

Alisema sigara hizo zenye bangi zinazoonekana katika mwonekano wa kutengenezwa kiwandani, zilikamatwa baada ya upekuzi uliofanywa kwa ushirikiano kati ya Jeshi la Polisi na maofisa wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) Idara ya Forodha katika mpaka huo. ACP Mallya alisema mzigo huo ulikuwa ukisafirishwa kwa basi la abiria la Kampuni ya Classic yenye namba za usajili za Jamhuri ya Kimodekrasia ya Kongo 6321AA25 ambalo lilikuwa likitokea Zimbabwe kwenda Dar es Salaam.

"Mabunda hayo yalikuwa yamefichwa nyuma ya kiti cha dereva yakiwa na mwonekano wa kipeto cha pakiti za sigara za kawaida zilizoandikwa Kkog Hybrid Malawi Gold," alisema.

Kamanda Mallya alisema kutokana na tukio hilo, jeshi hilo linamshikilia kondakta wa basi hilo, Vitalian Sanga (46) mkazi wa jijini Mbeya kwa mahojiano zaidi na ushahidi ukikamilika atafikishwa kwenye vyombo vya sheria.

Mallya alitoa wito kwa wananchi kuendelea kutoa taarifa za uhalifu ili matukio hayo yajulikane na kuthibitiwa.



Naibu Gavana wa kwanza wa Benki Kuu ya Congo, Dieudonné Fikiri Alimasi (wa pili kushoto), akikabidhi leseni kutoa huduma za kibenki katika nchi hiyo kwa Ofisa Mkuu wa Fedha Benki ya CRDB, Fredrick Nshekanabo (wa nne kushoto) na Mkurugenzi Mtendaji wa CRDB Congo, Jessica Nyachiro (wa nne kulia), katika hafla iliyofanyika nchini humo hivi karibuni. Wanaoshuhudia ni Mkuu wa Utawala wa Ubalozi wa Tanzania nchini Congo, Netho Yatega (wa tatu kushoto), Mkurugenzi wa Mawasiliano Benki ya CRDB na Mkurugenzi Mtendaji wa CRDB Bank Foundation, Tully Esther Mwambapa (wa tatu kulia), Mkurugenzi wa Hazina na Masoko ya Mitaji, Alex Ngusaru (wa pili kulia) na Mkuu wa Kitengo cha Huduma kwa Wateja Benki ya CRDB, Yolanda Uriyo (kulia) pamoja na maofisa wengine waandamizi wa benki hiyo. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# CRDB yapata leseni kufanya biashara DRC

**KINSHASA,** DRC

BENKI Kuu ya Congo (BCC) imeipatia leseni ya kufungua kampuni tanzu nchini humu Benki ya CRDB.

Leseni hiyo ilikabidhiwa juzi katika mkutano maalum kati ya BCC na ujumbe wa Benki ya CRDB ulioongozwa na Ofisa Mkuu wa Fedha wa Kundi, Fredrick Nshekanabo.

Akikabidhi leseni hiyo, Naibu Gavana wa Kwanza wa BCC, Dieudonné Alimasi, aliipongeza Benki ya CRDB kwa hatua hiyo muhimu. Itakayochochea ushindani katika sekta ya fedha nchini kwa kutambua kuwa benki hiyo ni moja ya benki zinazofanya vizuri katika ukanda wa Afrika Mashariki.

"Tulipopokea ombi lenu la kufungua kampuni tanzu hapa DRC, tulifurahi na tulilichukulia kwa umuhimu mkubwa hasa ukizingatia uhusiano uliopo baina ya nchi zetu. Niwapongeze kwa namna ambavyo mlikuwa mkitoa ushirikiano katika kila ambalo tuliwaambia kutekeleza. Hii inaonyesha jinsi gani mmedhamiria kuingia DRC na kufanya biashara hapa," alisema.

Katika taarifa yake kwa ujumbe wa Benki ya CRDB, Naibu Gavana pia alieleza kuwa BCC imepitisha mapendekezo ya uteuzi wa Jessica Nyachiro kama Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya CRDB nchini.

BCC pia imewaidhinisha DK. Fredrick Msemwa (Tanzania), Prof. Faustine Bee (Tanzania), Jeannot Okit'Otete (DRC), Olivier Duterme (DRC), Ornella Bomine (DRC) na Rama Bweya (DRC) kuwa Wajumbe wa Bodi ya Wakurugenzi wa Benki ya CRDB Congo.

Akizungumza wakati wa mkutano huo, Ofisa Mkuu wa Fedha wa Benki ya CRDB aliishukuru BCC kwa kuipatia benki hiyo leseni ya kufanya biashara nchini na kueleza kuwa Benki ya CRDB imeshafanya maandalizi yote ya kufungua milango nchini humo. Nshekanabo alimhakikishia Naibu Gavana kuwa Benki ya CRDB itashirikiana kwa karibu na BCC ili kusaidia kuimarisha sekta ya fedha DRC.

Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya CRDB Congo, Jessica Nyachiro alisema wamejipanga kikamilifu kuhakikisha wanatoa huduma bora na kwa ubunifu zitakazoendana na soko la DRC. Jessica alisema Benki ya CRDB itatumia uzoefu wake katika masoko ya Tanzania na Burundi kuhakikisha inakabiliana na ushindani nchini. Akieleza mkakati wa kufikisha uduma kwa wateja, Jessica alisema benki hiyo itaanza na tawi katika Mji wa Lubumbashi, huku akieleza kuwa katika mkakati wake wa biashara wa miaka mitatu inatazamia kupanua wigo wake katika miji mengine mikubwa ikiwamo Kinshasa, Lualaba, Kasai, Kisangani, Tanganyika na Kivu Kaskazini na Kusini.

"Benki yetu inasifika kwa uwekezaji mkubwa katika mifumo ya kidijitali, hivyo pamoja na mtandao wa matawi tunatarajia pia kutumia njia mbadala za ufikishaji huduma kama vile CRDB Wakala, SimBanking na Internet Banking kuwaunganisha wananchi wengi wa Congo katika huduma zetu," alisema Jessica.

Jessica aliongezea kuwa malengo ya Benki ya CRDB ni kuwa mshirika namba moja wa maendeleo DRC. Aliihakikishia serikali na wadau wa sekta binafsi nchini kuwa benki hiyo iko tayari katika kusaidia utekelezaji wa miradi mbalimbali ya kimkakati inayotekelezwa na sekta ya umma na binafsi.

"Benki yetu ina mizania kubwa ambayo inawezesha sekta zote za maendeleo. Kama ambavyo tumekuwa tukifanya Tanzania na Burundi huku pia tumejipanga kufanya hivyo," alisema huku akitoa mifano ya miradi ya reli ya kisasa (SGR) na ujenzi wa Bandari ya Kigoma ambayo benki hiyo inasaidia kuifadhili Tanzania. Ikikamilika itasaidia pia DRC. Jessica aliwashukuru Rais Samia Suluhu Hassan na Rais Felix Tshisekedi kwa kazi nzuri ya kuboresha uhusiano baina ya Tanzania na DRC ambao umesaidia kurahisisha benki hiyo kupata kibali nchini.

Israel Tshimanga Mutamba, Ofisa Uhusiano kwa Wateja wa Benki ya CRDB Congo aliwakaribisha wajasiriamali nchini, hususan vijana na wanawake kuchangamkia fursa zinazotolewa na benki hiyo huku akibainisha kuwa benki ina huduma mahsusi kwa ajili ya kundi hilo ikijumuisha mifumo ya kidijitali ya usimamizi wa biashara na mikopo nafuu.

Ujumbe wa Benki ya CRDB uliambatana na viongozi waandamizi wa Ubalozi wa Tanzania nchini Congo, wakiongozwa na Mkuu wa Utawala, Netho Yatega ambao wamekuwa sehemu ya mchakato mzima wa kuhakikisha benki hiyo inapata leseni ya kutoa huduma nchini.

# Mlalamikaji aomba kesi iondolewe mahakamani

**Na Grace Gurisha**

MKAZI wa Makongi wilayani Kinondoni, Dar es Salaam, Mussa Juma, ameiomba Mahakama ya Mwanzo Kariakoo kuiondoa kesi dhidi ya Rajabu Mbwana (63) anayetuhumiwa kumchoma kwa mkasi ubavuni kwa kuwa mshtakiwa ni kama baba yake.

Juma aliwasilisha ombi hilo jana mbele ya Hakimu Mkazi Mfawidhi wa mahakama hiyo, Claudis Kipande wakati kesi hiyo ilipoitwa kwa mara ya kwanza mahakamani huko.

Akisoma hati ya mashtaka, Karani Emmy Mwansasu alidai kuwa Mei Mosi, 2023, mshtakiwa Mbwana, saa 2:30 asubuhi, maeneo ya Ocean Road ndani ya Wilaya ya Ilala, alimshambulia Juma kwa kumchoma na mkasi ubavuni kushoto na mkononi.

Mshtakiwa Mbwana alipoulizwa na Hakimu Kipande kuhusu tuhuma hiyo ya shambulio la kudhuru mwili alikana kuhusika na tuhuma.

Baada ya mshtakiwa kukana shtaka hilo, mlalamikaji Juma aliiomba mahakama kuiondoa kesi hiyo kwa sababu Mbwana ni kama baba yake, hivyo amemsamehe.

Hakimu Kipande alikubaliana na ombi hilo la mlalamikaji na kumwachilia huru mshtakiwa.

# Wataalamu uandaaji miradi wanolewa Dar

**Na Maulid Mmbaga**

SERIKALI kwa kushirikiana na Shirika la Fedha la Kimataifa (IFC) imewakutanisha pamoja wataalamu wa kimataifa ambao wanahusika na utaalamu wa uandaaji wa miradi na mamlaka saba zikiwamo nne zinazohusika na sekta ya uchukuzi kwa lengo la kuwaongezea uelewa katika uandaaji na usimamiaji wa miradi nchini.

Akizungumza na waandishi wa habari juzi jijini Dar es Salaam wakati wa ufunguzi wa mafunzo hayo yatakayofanyika kwa siku tano, Kamishna wa Ubia Kati ya Sekta ya Umma na Binafsi (PPP), David Kafulila, alisema mafunzo hayo yatasaidia wataalamu wa ndani katika kujua ni namna ya kupanga na kutekeleza miradi ya ubia.

Alitaja mamlaka hizo nne ni Shirika la Reli (TRC), Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS), Mamlaka ya Bandari (TPA) na Mamlaka ya Viwanja vya Ndege (TIA). Kwa sekta ya nishati watazikutanisha Shirika la Umeme (TANESCO) na Wakala wa Nishati Vijijini (REA) pamoja na Mamlaka ya Mabasi Yaendayo Haraka (DART).

"Rais Samia Suluhu Hassan ni kinara katika kusukuma ajenda ya sekta binafsi kuhakikisha inatoa mchango kwenye kuendesha uchumi. Inafahamika kwamba sekta binafsi ndiyo injini ya uchumi, na kwenye ubia kati ya sekta ya umma na binafsi msingi wake ni binafsi itekeleze baadhi ya maeneo ambayo serikali ingeyatekeleza.

"Lengo la mafunzo hayo ni kubadilishana uzoefu na kujenga uwezo wa mamlaka zetu ili zitekeleze miradi mikubwa. Tunayo nafasi na fursa kubwa ya kutekeleza miradi mikubwa TANESCO, TANROADS na maeneo mengine," alisema Kafulila.

Alieleza kuwa kwa sasa Kitengo cha PPP na TANESCO wanashirikiana katika miradi mitatu ya uzalishaji wa umeme kwa njia ya jua wilayani Same mkoani Kilimanjaro, Singida na Dodoma, miradi hiyo ikigharimu dola milioni 300 takribani Sh. bilioni 657.

Pia alibainisha kuwa wanaitumia fursa ya sekta binafsi kupunguza mzigo wa deni la serikali na ulazima wa kodi kutumika kutekeleza miradi ambayo inaweza kutekelezwa na sekta binafsi.

"Tunajenga miungombinu hii kwa utaratibu wa ubia lakini tutakuwa na wajibu wa kulipia huduma hiyo ili upunguze hasara ambayo ungeipata kwa kutotumia hiyo huduma, ukikaa barabarani kwenye foleni inaweza kukugharimu mafuta mengi zaidi kuliko gharama utakayoitumia kulipa ili upite kwenye 'Express way'," alisema Kafulila. Mkurugenzi Mkazi wa IFC, Frank Ajilore, aliihakikishia serikali, shirika hilo litakuwa mshirika katika kuendeleza na kufanikisha ajenda ya PPP nchini.

Alisema IFC ina uwezo wa kuwaweka pamoja watu ambao watashughulika katika kutafuta mtaji wa miradi ya ubia inayotaka kutekelezwa nchini.

"Kuna wataalamu watakuja na kujumuika katika mafunzo haya, lengo ni kuanza kuandaa miradi ambayo itakuwa kwenye orodha ya ile itakayotekelezwa kupitia ubia. IFC pia ina uwezo wa kufanya kazi na watu kutoka kwenye masoko ya mtaji na kuongeza uwezo wa benki na watoa mitaji katika mitaji wanayoitoa hasa kwenye kuiongezea muda," alisema Ajilore.

HABARI KITAIFA

# Wasafirishaji, wachumi watoa angalizo kupaa bei ya mafuta

**Na Elizabeth Zaya**

BAADHI ya watumiaji wa bidhaa za mafuta na wachumi nchini wamesema kupanda na kushuka kwa bei ya mafuta si jambo zuri katika uchumi, wakikutaja kunasababisha mfumuko wa bei za bidhaa.

Juzi Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA) ilitangaza bei mpya za mafuta huku bei ya mafuta ya petroli na dizeli zikipaa kwa yale yanayoingia kupitia Bandari ya Dar es Salaam kulinganishwa na mwezi Aprili.

Mkurugenzi Mtendaji wa Taasisi ya Utafiti (REPOA), Dk. Donald Mmari, alisema kushuka na kupanda kwa mafuta siyo jambo zuri katika uchumi kwa kuwa kwa kiwango kikubwa husababisha bidhaa kupanda.

"Shida ni kwamba, baadhi ya bidhaa zinapopanda huwa hazishuki.

Kwa hiyo, hali hii huleta athari kwenye uchumi hasa kwa wananchi," alisema Dk. Mmari.

Alisema ni vyema kuwapo mikakati ya kuwa na akiba ya nishati hiyo ili kuepuka kupanda na kushuka kwa nishati hiyo.

Chama cha Wamiliki wa Mabasi (TABOA), kilisema jana kuwa kupanda kwa bei ya mafuta kunaathiri uendeshaji.

"Kupanda kwa mafuta kunatuathiri moja kwa moja kwa sababu bei ya nauli ya mabasi huwa inachukua muda mrefu kuridhiwa na serikali. Kwa hiyo, bei ya mafuta inaongezeka na nauli zinabaki palepale.

"Kwa hiyo gharama za uendeshaji zinakuwa kubwa na faida inakuwa hakuna na biashara inakuwa ngumu," alisema Priscus Joseph, Katibu Mtendaji wa TABOA.

Agnes Charles, anayemiliki gari binafsi, alisema kupanda na kushuka kwa mafuta kunamwathiri kwa sababu wakati mwingine hulazimika kuliacha na kutumia usafiri mwingine katika shughuli zake za kumwingizia kipato kutokana na kushindwa kumudu gharama.

"Hili ni tatizo kwa sababu ndani ya vipindi vifupi mafuta yanapanda, inakuwa ni gharama kubwa kutumia gari kwenye mizunguko yangu ya kutafuta fedha na wakati mwingine inanilazimu kuacha gari kwa muda muda," alilalamika.

Dereva wa bodaboda aliyejitaja kwa jina moja la Aidan, mwenye kituo cha kazi eneo la ITV, Kinondoni, alisema yanapopanda hulazimika kupandisha nauli na athari wanazokutana nazo ni kupungua kwa abiria.

"Wengine bodaboda tunazoendesha si za kwetu, tunapeleka hesabu kila siku kwa bosi. Kwa hiyo, mafuta yanapopanda inakuwa ngumu kwetu kwa sababu ni lazima tupandishe nauli maana bila kufanya hivyo hupati faida, tunapopandisha tunashindwa kufanya kazi," alisema.

Katika taarifa ya EWURA iliyotolewa na Mkurugenzi Mkuu wake, Dk. James Mwainyekule, mafuta yanayoingia kupitia Bandari ya Dar es Salaam, petroli yatauzwa Sh. 2,871 mwezi huu kutoka Sh. 2,781 iliyouzwa mwezi Aprili.

Bei ya dizeli imeongezeka kutoka Sh. 2,847 Aprili hadi Sh. 2,871 mwezi huu, sawa na ongezeko la Sh. 24.




Wafanyakazi wa Kampuni ya Sukari ya Kilombero na viongozi wa Chama cha Wafanyakazi wa Mashamba na Kilimo Tanzania (TPAWU), wakionyesha mshikamano wakati wa kufunga maonyesho ya Siku ya Usalama na Afya Mahali pa Kazi Duniani mjini Morogoro hivi karibuni. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Baada ukimya, Prof. Jay ajitokeza akiwashukuru CCM na CHADEMA

**Na Jenifer Gilla**

ALIYEKUWA Mbunge wa Mikumi, Joseph Haule, maarufu Profesa Jay, amejitokeza kwa mara ya kwanza baada ya kuugua kwa takribani mwaka mmoja na kuwashukuru wadau, akiwamo Rais Samia Suluhu Hassan, kwa kugharamia matibabu yake.

Viongozi wengine aliowashukuru ni pamoja na wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) na wadau ambao walijitoa wakati wote wa matibabu yake. Januari 30 mwaka jana, Profesa Jay alifikishwa katika Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH) akiwa katika hali mbaya kiafya na kukaa katika Chumba cha Uangalizi Maalum (ICU) kwa siku 127 na baadaye kuendelea na matibabu ya kawaida hospitalini huko.

Kutokana na hali hiyo, CHADEMA kwa kushirikiana na vyombo vya habari na wadau wengine walihamasisha jamii kumchangia fedha za matibabu mpaka Februari 11, mwaka jana, serikali ilipobeba jukumu la kugharamia matibabu hayo.

Kupitia ukurasa wake wa kijamii wa Instagram, mbunge huyo ameandika ujumbe, akitoa shukrani zake kwa Rais Samia kwa kugharamia matibabu yake katika hospitali hiyo na nje ya nchi. "Ahsante sana Mama (Samia) pamoja na serikali yako yote, kwani viongozi wako wa chama na serikali walikuwa wanapishana kuja kuniona na kunifariji," inasomeka sehemu ya ujumbe.

Vilevile, aliwashukuru wanachama wa CHADEMA wakiongozwa na Mwenyekiti wa chama hicho, Freeman Mbowe, kwa kushirikiana na serikali kuhakikisha anapata matibabu bora.

Pia aliwashukuru madaktari na manesi wa Muhimbili na hospitali zingine alizopita kwa kumpa matibabu ya kiwango cha juu kwa mwaka mzima aliolazwa na siku 127 alizokuwa ICU.

"Mwisho kwa umuhimu mkubwa ninawashukuru sana Watanzania wote kwa kujitolea kwa maombi na michango ya fedha zetu kuhakikisha ninatibiwa, na kusema ukweli ilinisaidia sana kulipia gharama za matibabu za awali kabla serikali kuamua kuingilia kati," anasema Profesa Jay aliyeweka picha yake mpya baada ya kupitia madhila hayo.

Mbunge huyo wa zamani wa Mikumi aliwashukuru waliosimamia na kuhamasisha ukusanyaji wa michango hiyo vikiwamo vyombo vya habari, viongozi wa dini zote waliojitolea kumwombea, mke wake, ndugu, jamaa na marafiki kwa upendo mkubwa waliouonyesha wakati anaumwa.

# NBC yazindua kampeni mpya

**Na Halfan Chusi**

BENKI ya NBC imezindua kampeni mpya inayoitwa 'Shinda Mechi Zako na NBC', ikilenga kuwawezesha wateja wake kutimiza malengo yao ya kiuchumi na kijamii kupitia akaunti na huduma mbalimbali inazozitoa na kuunga mkono mikakati ya serikali kukuza uchumi jumuishi.

Uzinduzi wa kampeni hiyo ulifanyika jana jijini na Dar es Salaam na kuhudhuriwa na wadau mbalimbali wakiwamo wajasiriamali, waendesha pikipiki, mawakala wa benki hiyo na wadau wa michezo.

Akizungumza wakati wa hafla hiyo, Mkuu wa Bidhaa za NBC, Abel Kaseko, alisema kampeni hiyo inalenga wateja binafsi, waajiriwa, wamiliki wa biashara ndogo, mawakala na watu wengine wanaotumia huduma za benki za kimtandao kupitia NBC.

"Kupitia kampeni hii, tunalenga kuwasaidia wateja wetu kwa kuwaongezea thamani ili watimize malengo yao ya kiuchumi na kijamii na pia kuchangia katika ukuaji wa uchumi binafsi na wa taifa kwa ujumla.

"Kwa kutambua changamoto mbalimbali zinazowakabili watu wa aina zote, NBC tumejipanga kuwasaidia kutatua changamoto hizo kupitia ushauri na huduma za kifedha. Tumezifananisha changamoto hizo na mechi za mchezo wa mpira wa miguu na hiyo ndio sababu ya kampenii kufahamika kwa jina 'Shinda Mechi Zako na NBC'," alisema.

Kupitia kampeni hiyo, benki hiyo inatoa miamala, kulipia kwa kadi huduma za mtandaoni kwa punguzo la bei, na upatikanaji wa mikopo binafsi na ya biashara hadi Sh. milioni 150 ndani ya saa 48.

"Wateja wetu pia wanaweza kupata faida ya hadi asilimia saba kwenye akaunti zao za NBC Malengo. Wateja wanaweza pia kupata mkopo wa kumalizia nyumba kwa gharama nafuu ili kukamilisha ndoto zao za ujenzi wa nyumba," alisema.

Mkuu wa Masoko ya NBC, David Raymond alisema kampeni hiyo itasaidia mikakati ya serikali kutoa huduma za kifedha na kukuza uchumi wa Watanzania.

# MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

## Waliohusika na fedheha hii wasionewe huruma asilani

**KATIKA** moja ya habari kwenye gazeti hili ni kutelekezwa kwa zaidi ya wafanyakazi na wanachama 70 wa Chama cha Wafanyakazi wa Serikali za Mitaa Tanzania (TALGWU) baada ya kumalizika kwa maadhimisho ya Siku ya Wafanyakazi Duniani (Mei Mosi) katika Uwanja wa Kumbukumbu ya Sokoine jijini Mbeya.

Wanachama hao, kwa mujibu wa taarifa hiyo, walitarajia kulipwa posho ambazo pia zingewasaidia kupata chakula kutokana na kuhudhuria maadhimisho hayo kutoka kwa viongozi wa chama chao. Kinyume cha matarajio hayo, walijikuta wamebaki uwanjani wasijue la kufanya baada ya viongozi wao kuingia mitini.

Miongoni mwa wafanyakazi hao waliotelekezwa ni watendaji wa vijiji na kata, maofisa kilimo na wa idara ya afya. Hata baada ya kumalizika kwa sherehe hizo, walipotakiwa waondoke uwanjani hapo na kurejea nyumbani, waligoma huku wakitaka viongozi wao wawalipe ndipo watawanyike. Walikubali kuondoka baada ya viongozi wa TALGWU mkoa na wale wa serikali kuingilia kati.

Watumishi hao, wakizungumza na vyombo vya habari, walisema viongozi wao waliwatoroka na kuwaacha bila kuwapa nauli za kurudi kwenye vituo vyao vya kazi ilhali wenzao wa wilaya zote za mkoa wa Mbeya walilipwa.

Kitu cha kushangaza na kuonyesha viongozi hao hawana hata chembe ya huruma ni pale walipoondoka eneo la sherehe na kuzima simu zao. Hatua hiyo ilionyesha ni unyama uliopitiliza dhidi ya binadamu wenzao ambao ni wanachama wanaochangia mfuko wa chama kutoka kwenye mishahara yao ya kila mwezi.

Mmoja wa wanachama hao, alikaririwa na waandishi wa habari akisema viongozi hao waliwaahidi kuwa kila atakayehudhuria atalipwa posho na kupewa chakula cha mchana. Swali la kujiuliza ni je, nini sababu ya viongozi hao kuondoka na fedha ambazo ni haki ya wafanyakazi ambao wamekuwa wakichangia kutoka kwenye vipato vyao?

Lakini pia jambo la kushangaza, kama alivyosema mwanachama huyo ni kwamba kila mwaka wanapohudhuria sherehe hizo, wamekuwa wakilipwa Sh. 2,500. Ni hali mwanachama anayechangia sehemu ya mshahara wake kupewa kiasi hicho cha fedha? Je, mamilioni ya fedha yanayochangwa na kubaki katika wilaya husika yanafanya kazi gani?


Kwa ujumla, kitendo kilichofanywa na viongozi hao wa TALGWU wilaya ya Mbeya ni cha fedheha na udhalilishaji ambacho kinapaswa kukemewa na kulaaniwa na chama hicho ngazi ya mkoa na taifa pamoja na Shirikisho la Wafanyakazi Tanzania (TUCTA).

Ni imani kwamba viongozi waliohusika na udhalilishaji wa wafanyakazi ambao huwakiwa na jua au kunyeshewa na mvua wakati wa maadhimisho hayo, watachukuliwa hatua na viongozi wao ngazi za juu ili iwe fundisho kwa wengine wenye tabia kama hizo na wale wanaotafuna fedha za michango ya wafanyakazi kwa ajili ya maendeleo ya taasisi.

Pamoja na hayo, kitendo hicho kimedhihirisha kuwa baadhi ya viongozi wanaoingia kwenye vyama vya wafanyakazi, hawana nia thabiti ya kutetea maslahi ya wafanyakazi ambayo yamekuwa kilio kila mwaka wakati maadhimisho hayo yanapofanyika bali kinachowasukuma ni maslahi yao binafsi.

Aidha, kitendo hicho kimefumbua macho wadau wengi wa masuala ya wafanyakazi na nchi kwa ujumla kuwa unapaswa kufanyika ukaguzi wa fedha na mali za vyama hivyo, ikiwezekana kazi hiyo ifanywe na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG). Ni imani kwamba iwapo kazi hiyo itafanyika, yataibuliwa madudu mengi yanayoweza kuwaanika wahusika na wengine kufikishwa katika vyombo vya sheria.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



## Tuwe makini na wizi wa mitihani, tusipoziba ufa, tutajenga ukuta

Na Adolf F. Mkenda

**MITIHANI** ya mwisho ya kidato cha sita nchini, imeanza rasmi tarehe mbili mwezi huu wa tano na itakamilika tarehe 22 ya mwezi huu. Mitihani hii itafanyika, sambamba na mitihani ya wanafunzi wanaosomea ualimu.

Kadhalika, wapo wanafunzi ambao matokeo yao ya kidato cha nne yalifutwa na wameruhusiwa kurudia mitihani yao katika kipindi hiki cha mitihani. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dk. Samia Suluhu Hassan, kupitia akaunti yake ya 'Twitter' ametuma salamu za heri kwa watahiniwa wote.

Mimi, pamoja na wenzangu wote kwenye Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia tunaungana na Rais wetu kuwatakia watahiniwa wote kila la heri kwenye mitihani hii.

Pamoja na salamu hizi, natoa wito kwa watahiniwa wote kuzingatia masharti na taratibu zote za mitihani. Kutokuzingatia masharti ya mitihani kunaweza kupelekea mtahiniwa kufutiwa matokeo yake ya mitihani. Walimu, wasimamizi wa mitihani, wazazi na walezi wote kwa pamoja, tuhimize watahiniwa wetu wafanye mitihani yao kwa kuzingatia masharti na taratibu zilizowekwa.

Napenda kutumia fursa hii, pia kutoa wito kwa Watanzania wote tushirikiane kutokomeza udanganyifu na wizi wa mitihani. Ni kweli kwamba, tatizo la wizi na udanganyifu wa mitihani ni dogo sana hapa nchini, lakini tusipoziba ufa tutajenga ukuta. Tutakosea sana, tukifumbia macho tatizo hili hata kama ni dogo sana. Kufumbia macho na kunyamaza hakuondoi tatizo. Kuficha tatizo na kutokuchukua hatua madhubuti ni sawa na kulea na kukuza tatizo.

Madhara ya kuenea kwa wizi na udanganyifu wa mitihani ni makubwa sana kwa taifa letu. Kwanza, wizi na udanganyifu wa mitihani unaathiri haki za watahiniwa wanaofanya mitihani yao kwa uadilifu.

Kwa kawaida, wizi na udanganyifu wa mitihani unaoratibiwa na watumishi wasio waaminifu, hunufaisha watahiniwa wenye uwezo zaidi wa kifedha; wenye uwezo mdogo wa kiuchumi hawawezi kulipa gharama za mitihani ya wizi.

Pili, wizi na udanganyifu wa mitihani unadumaza weledi katika taifa letu na kukuza ubabaishaji. Hatimaye, tutakuwa na madaktari wababaishaji, marubani wababaishaji, walimu wababaishaji na kadhalika.

Tatu, wizi na udanganyifu wa mitihani unaharibu malezi ya watoto na vijana wetu kwa kufundisha wizi na udanganyifu kwamba njia ya kutafuta mafanikio. Serikali itaendelea kuchukua hatua kali dhidi ya wote wanaojihusisha na wizi na udanganyifu wa mitihani.

Tunao maofisa ambao wako mahabusu wakikabiliwa na mashtaka ya madai ya kuratibu na kuwezesha wizi na udanganyifu wa mitihani. Zipo baadhi ya shule ambazo zimefutwa kama vituo vya mitihani kwa sababu ya wizi na udanganyifu wa mitihani.

Endapo itatulazimu, tutafuta usajili wa shule zinazoratibu wizi na udanganyifu wa mitihani. Ni matumaini yetu kwamba hatutalazimika kufuta usajili wa shule, lakini ni vyema ikafahamika kuwa hii ni hatua inayoweza kuchukuliwa.

Endapo sote tutashikamana na kukemea udanganyifu kwenye mitihani hapana shaka tutafanikiwa kutokomeza jambo hili.

Ni jukumu la kila mmoja wetu kuwa macho na kutoa taarifa endapo tutaona dalili zozote za udanganyifu kwenye mitihani. Mtu yeyote atakayekuwa na taarifa kuhusu vitendo vya wizi na udanganyifu wa mitihani tunamwomba atoe taarifa kwa mamlaka yoyote ya serikali iliyo karibu naye.

Namba ya simu ifuatayo itatumika pia kupokea taarifa zozote kwa siri za wizi na udanganyifu wa mitihani: Taarifa zinaweza kutumwa kwa simu 0759 360 000 na namba barua pepe ifuatayo:esnecta@necta.go.tz. Mwisho napenda tena kuwatakiwa watahiniwa wote kila la heri katika mitihani yao.

**• Mwandishi ni Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia.**

## MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Waliohusika na fedheha hii wasionewe huruma asilani

**KATIKA** moja ya habari kwenye gazeti hili ni kutelekezwa kwa zaidi ya wafanyakazi na wanachama 70 wa Chama cha Wafanyakazi wa Serikali za Mitaa Tanzania (TALGWU) baada ya kumalizika kwa maadhimisho ya Siku ya Wafanyakazi Duniani (Mei Mosi) katika Uwanja wa Kumbukumbu ya Sokoine jijini Mbeya.

Wanachama hao, kwa mujibu wa taarifa hiyo, walitarajia kulipwa posho ambazo pia zingewasaidia kupata chakula kutokana na kuhudhuria maadhimisho hayo kutoka kwa viongozi wa chama chao. Kinyume cha matarajio hayo, walijikuta wamebaki uwanjani wasijue la kufanya baada ya viongozi wao kuingia mitini.

Miongoni mwa wafanyakazi hao waliotelekezwa ni watendaji wa vijiji na kata, maofisa kilimo na wa idara ya afya. Hata baada ya kumalizika kwa sherehe hizo, walipotakiwa waondoke uwanjani hapo na kurejea nyumbani, waligoma huku wakitaka viongozi wao wawalipe ndipo watawanyike. Walikubali kuondoka baada ya viongozi wa TALGWU mkoa na wale wa serikali kuingilia kati.

Watumishi hao, wakizungumza na vyombo vya habari, walisema viongozi wao waliwatoroka na kuwaacha bila kuwapa nauli za kurudi kwenye vituo vyao vya kazi ilhali wenzao wa wilaya zote za mkoa wa Mbeya walilipwa.

Kitu cha kushangaza na kuonyesha viongozi hao hawana hata chembe ya huruma ni pale walipoondoka eneo la sherehe na kuzima simu zao. Hatua hiyo ilionyesha ni unyama uliopitiliza dhidi ya binadamu wenzao ambao ni wanachama wanaochangia mfuko wa chama kutoka kwenye mishahara yao ya kila mwezi.

Mmoja wa wanachama hao, alikaririwa na waandishi wa habari akisema viongozi hao waliwaahidi kuwa kila atakayehudhuria atalipwa posho na kupewa chakula cha mchana. Swali la kujiuliza ni je, nini sababu ya viongozi hao kuondoka na fedha ambazo ni haki ya wafanyakazi ambao wamekuwa wakichangia kutoka kwenye vipato vyao?

Lakini pia jambo la kushangaza, kama alivyosema mwanachama huyo ni kwamba kila mwaka wanapohudhuria sherehe hizo, wamekuwa wakilipwa Sh. 2,500. Ni hali mwanachama anayechangia sehemu ya mshahara wake kupewa kiasi hicho cha fedha? Je, mamilioni ya fedha yanayochangwa na kubaki katika wilaya husika yanafanya kazi gani?


Kwa ujumla, kitendo kilichofanywa na viongozi hao wa TALGWU wilaya ya Mbeya ni cha fedheha na udhalilishaji ambacho kinapaswa kukemewa na kulaaniwa na chama hicho ngazi ya mkoa na taifa pamoja na Shirikisho la Wafanyakazi Tanzania (TUCTA).

Ni imani kwamba viongozi waliohusika na udhalilishaji wa wafanyakazi ambao huwakiwa na jua au kunyeshewa na mvua wakati wa maadhimisho hayo, watachukuliwa hatua na viongozi wao ngazi za juu ili iwe fundisho kwa wengine wenye tabia kama hizo na wale wanaotafuna fedha za michango ya wafanyakazi kwa ajili ya maendeleo ya taasisi.

Pamoja na hayo, kitendo hicho kimedhihirisha kuwa baadhi ya viongozi wanaoingia kwenye vyama vya wafanyakazi, hawana nia thabiti ya kutetea maslahi ya wafanyakazi ambayo yamekuwa kilio kila mwaka wakati maadhimisho hayo yanapofanyika bali kinachowasukuma ni maslahi yao binafsi.

Aidha, kitendo hicho kimefumbua macho wadau wengi wa masuala ya wafanyakazi na nchi kwa ujumla kuwa unapaswa kufanyika ukaguzi wa fedha na mali za vyama hivyo, ikiwezekana kazi hiyo ifanywe na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG). Ni imani kwamba iwapo kazi hiyo itafanyika, yataibuliwa madudu mengi yanayoweza kuwaanika wahusika na wengine kufikishwa katika vyombo vya sheria.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



# Tuwe makini na wizi wa mitihani, tusipoziba ufa, tutajenga ukuta

Na Adolf F. Mkenda

**MITIHANI** ya mwisho ya kidato cha sita nchini, imeanza rasmi tarehe mbili mwezi huu wa tano na itakamilika tarehe 22 ya mwezi huu. Mitihani hii itafanyika, sambamba na mitihani ya wanafunzi wanaosomea ualimu.

Kadhalika, wapo wanafunzi ambao matokeo yao ya kidato cha nne yalifutwa na wameruhusiwa kurudia mitihani yao katika kipindi hiki cha mitihani. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dk. Samia Suluhu Hassan, kupitia akaunti yake ya 'Twitter' ametuma salamu za heri kwa watahiniwa wote.

Mimi, pamoja na wenzangu wote kwenye Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia tunaungana na Rais wetu kuwatakia watahiniwa wote kila la heri kwenye mitihani hii.

Pamoja na salamu hizi, natoa wito kwa watahiniwa wote kuzingatia masharti na taratibu zote za mitihani. Kutokuzingatia masharti ya mitihani kunaweza kupelekea mtahiniwa kufutiwa matokeo yake ya mitihani. Walimu, wasimamizi wa mitihani, wazazi na walezi wote kwa pamoja, tuhimize watahiniwa wetu wafanye mitihani yao kwa kuzingatia masharti na taratibu zilizowekwa.

Napenda kutumia fursa hii, pia kutoa wito kwa Watanzania wote tushirikiane kutokomeza udanganyifu na wizi wa mitihani. Ni kweli kwamba, tatizo la wizi na udanganyifu wa mitihani ni dogo sana hapa nchini, lakini tusipoziba ufa tutajenga ukuta. Tutakosea sana, tukifumbia macho tatizo hili hata kama ni dogo sana. Kufumbia macho na kunyamaza hakuondoi tatizo. Kuficha tatizo na kutokuchukua hatua madhubuti ni sawa na kulea na kukuza tatizo.

Madhara ya kuenea kwa wizi na udanganyifu wa mitihani ni makubwa sana kwa taifa letu. Kwanza, wizi na udanganyifu wa mitihani unaathiri haki za watahiniwa wanaofanya mitihani yao kwa uadilifu.

Kwa kawaida, wizi na udanganyifu wa mitihani unaoratibiwa na watumishi wasio waaminifu, hunufaisha watahiniwa wenye uwezo zaidi wa kifedha; wenye uwezo mdogo wa kiuchumi hawawezi kulipa gharama za mitihani ya wizi.

Pili, wizi na udanganyifu wa mitihani unadumaza weledi katika taifa letu na kukuza ubabaishaji. Hatimaye, tutakuwa na madaktari wababaishaji, marubani wababaishaji, walimu wababaishaji na kadhalika.

Tatu, wizi na udanganyifu wa mitihani unaharibu malezi ya watoto na vijana wetu kwa kufundisha wizi na udanganyifu kwamba njia ya kutafuta mafanikio. Serikali itaendelea kuchukua hatua kali dhidi ya wote wanaojihusisha na wizi na udanganyifu wa mitihani.

Tunao maofisa ambao wako mahabusu wakikabiliwa na mashtaka ya madai ya kuratibu na kuwezesha wizi na udanganyifu wa mitihani. Zipo baadhi ya shule ambazo zimefutwa kama vituo vya mitihani kwa sababu ya wizi na udanganyifu wa mitihani.

Endapo itatulazimu, tutafuta usajili wa shule zinazoratibu wizi na udanganyifu wa mitihani. Ni matumaini yetu kwamba hatutalazimika kufuta usajili wa shule, lakini ni vyema ikafahamika kuwa hii ni hatua inayoweza kuchukuliwa.

Endapo sote tutashikamana na kukemea udanganyifu kwenye mitihani hapana shaka tutafanikiwa kutokomeza jambo hili.

Ni jukumu la kila mmoja wetu kuwa macho na kutoa taarifa endapo tutaona dalili zozote za udanganyifu kwenye mitihani. Mtu yeyote atakayekuwa na taarifa kuhusu vitendo vya wizi na udanganyifu wa mitihani tunamwomba atoe taarifa kwa mamlaka yoyote ya serikali iliyo karibu naye.

Namba ya simu ifuatayo itatumika pia kupokea taarifa zozote kwa siri za wizi na udanganyifu wa mitihani: **Taarifa zinaweza kutumwa kwa simu 0759 360 000 na namba barua pepe ifuatayo:esnecta@necta.go.tz. Mwisho napenda tena kuwatakiwa watahiniwa wote kila la heri katika mitihani yao.**

**• Mwandishi ni Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia.**

# Wadai kulipwa ujira mdogo kiwandani

**Na Enock Charles**

WAFANYAKAZI wa kiwanda cha vioo cha Keda kilichoko Kijiji cha Mbezi Msufini, Kata ya Mkuranga mkoani Pwani, wamelalamikia ujira mdogo wanaolipwa na mwekezaji wa kiwanda hicho, wakidai hautoshelezi mahitaji yao kutokana na kupanda kwa gharama za maisha.

Wamedai kuwa bei za bidhaa, hasa vyakula kwa sasa ziko juu na hivyo wanaiomba serikali kuingilia kati ili waongezwe ujira.

Wakizungumza na waandishi wa habari kijijini huko mwanzoni mwa wiki, wafanyakazi hao walidai kuwa ujira wa Sh. 6,000 wanaolipwa kwa siku ni mdogo na hivyo kutaka uongezwe ili kuendana na hali ya maisha ya sasa.

"Sisi ni wafanyakazi wa mle ndani, kero yetu sisi vibarua ni ya malipo; kwanza ni kidogo na hatulipwi kwa wakati," alisema Ramadhani Mkali, aliyejitambulisha ni miongoni mwa wafanyakazi wa kiwanda hicho. Aliendelea kudai kuwa: "Awali walituambia kwamba watatulipa kwa wiki lakini cha ajabu ni kwamba ikifika hiyo wiki, hawatulipi. Zinapita hata siku tatu mbele ndipo wanatulipa."

Alidai kero yao ya pili ni kutoruhusiwa kufanya kazi baadhi ya siku, hasa kipindi cha mvua, akifafanua "unakuta wanachagua wafanyakazi wao waliotoka Chalinze, Sasa sisi tunarudi vipi tena nyumbani wakati ni wafanyakazi wa mle tumejitoa kufanya kazi na ndiyo tunayoitegemea halafu unafika unaambiwa rudi nyumbani?"

Alipotafutwa na Nipashe juzi kuzungumzia suala hilo, Meneja Rasilimaliwatu wa kampuni hiyo, Hussein Juma, alisema wameajiri wafanyakazi wengi na kuna tofauti ya malipo kulingana na ujuzi wa mtu. Kuhusu madai ya baadhi ya vibarua kuzuia kufanya kazi kwa baadhi ya siku, Juma alisema hayana ukweli kwa kuwa wanahudumiwa wote kwa usawa bila kujali walikotoka.

"Mtu anayelipwa Sh. 100,000 kwa siku, hawasemi kuna injinia tumemuajiri analipwa zaidi ya Sh. 120,000 kwa siku. Hawasemi, dereva analipwa Sh. 35,000 kwa siku, hawasemi!

"Pia wamezungumzia kipindi cha mvua, kipindi cha mvua uzalishaji unakuwa mdogo. Sasa utengeneze orodha ya malipo ya Sh. milioni tatu au nne halafu hakuna kilichofanyika!" Alifafanua.

Mwenyekiti wa kijiji hicho, Ibrahim Thabit, alisema serikali ilitangaza fursa ya ajira kwa wananchi kuchangamkia fursa za kuwapo kwa kiwanda hicho.

Alisema wapo waliokubali na wengine walikataa ujira huo kwa kuwa wanazo kazi zinazowapa kipato zaidi ya hicho.

Kwa mujibu wa mwongozo wa wizara yenye dhamana ya kazi, vijana, ajira na watu wenye ulemavu kuhusu malipo ya wafanyakazi viwandani uliotolewa mwaka jana, kima cha chini cha malipo kwa siku ni kwa wafanyakazi na vibarua wa viwandani ni Sh. 5,770.

Mwongozo huo pia unatamka kuwa mfanyakazi kucheleweshewa malipo ni kosa kisheria.




Ofisa Rasilimali Watu wa Kampuni ya Barrick North Mara, Gema Salamba, akizungumza na wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Mzumbe mkoani Morogoro, wakati wa kongamano la kuwajengea uwezo wa kuibua vipaji na kuchangamkia fursa lililoandaliwa na Taasisi ya AIESEC na kufanyika juzi kwa udhamini wa kampuni hiyo. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Kambaya aondoka CHADEMA baada ya siku 53 kisa ahadi

**Na Christina Mwakangale**

ABDUL Kambaya ametangaza kujiondoa katika Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), ikiwa ni siku 53 tangu yeye na wanachama wengine 384 walipojiunga na chama hicho cha siasa wakitokea Chama cha Wananchi (CUF) Machi 11, mwaka huu.

Hata hivyo, Mkurugenzi wa Itifaki, Mawasiliano na Mambo ya Nje wa CHADEMA, John Mrema, aliiambia Nipashe jana kuwa chama chao hakina taarifa rasmi kuhusu kuondoka kwa mwanachama huyo mpya.

Akizungumza na Nipashe jana, Kambaya ambaye hakuwa tayari kusema anakoelekeza nguvu zake kisiasa wala idadi kamili ya wanachama walioko nyuma yake, alidai sababu kuu ya kufanya hivyo ni kutotimizwa kwa ahadi aliyopewa na CHADEMA wakati anaondoka CUF.

"Changamoto zimejitokeza, unaamua bora ukae pembeni, usionekane kwamba wewe ndiyo mwanzisha mgogoro. CHADEMA mimi sio kiongozi, hata wa ngazi ya tawi. Watu ulioondoka nao wanakusukuma kwamba 'sisi tuliahidiwa hiki na hiki'.

"Waliokuahidi 'njoo mtagombea ubunge', wanaendelea na kampeni za kuutafuta ubunge wao wenyewe. Sasa ukibaki hapo si utakuwa mtihani? Bora uache siasa ukae pembeni," alisema Kambaya.

Alisema wanachama walioondoka CUF na kujiunga na CHADEMA waliomba wapatiwe ofisi, lakini ombi lao halijatekelezwa zaidi ya wanachama hao kutakiwa kuchangia Sh. 2,500 ili kupata kadi na kisha kushiriki uchaguzi wa ndani ya chama.

"Kuna mazingira magumu. Mimi niliahidiwa hapa Kinondoni, niliahidiwa njoo, tunakutafuta ugombee ubunge. Huyo huyo aliyenifuata anaanza kujipanga kugombea. Tangu sisi tumeingia ndani ya chama (CHADEMA), harakati za uchaguzi zipo zinaendelea, tuliotangaza leo (jana) ninafikiri tunafikia 10 ila wiki ijayo watatangaza wengine," alisema Kambaya. Pamoja na uamuzi wake na wanachama wenzake wa kuondoka CHADEMA, Kambaya alidai kwamba bado anakiona ni chama makini kimtazamo kulinganishwa na vingine.

"Chama makini ni huko tulikotoka (CHADEMA) na si kingine, lakini matatizo ni hayo. Siwezi kwenda ACT-Wazalendo na CCM haiwezekani. Siwezi kujiunga kwenye chama chochote.

"Ninaondoka CHADEMA na sitojiunga na chama chochote. Kwa sasa mimi ni mwanasiasa huru," alisema.

Machi 11, mwaka huu, wanachama 384 walijiunga rasmi na CHADEMA baada ya kutangaza kujitoa CUF. Kati yao, ni Kambaya ambaye alikuwa Mkurugenzi wa Habari na Uenezi wa CUF.

Mwenyekiti wa CHADEMA, Freeman Mbowe, ndiye aliyewakaribisha wanachama hao waliotoka CUF, akisema wana haki sawa na mwanachama mwingine yeyote ndani ya CHADEMA

**KABWELA** — **Na Fadhili Mohammed**



# Gwajima ataka mamlaka kusimamia mifugo, uvuvi

**Na Gwamaka Alipipi,** DODOMA

MBUNGE wa Kawe, Josephat Gwajima, amesema ili sekta za uvuvi na mifugo zitoe mchango mkubwa katika Pato la Taifa ni lazima ianzishwe mamlaka itayozisimamia na kuwa na dira itakayotoa mwelekeo.

Alitoa ushauri huo jana bungeni jijini Dodoma alipochangia makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa mwaka wa fedha 2023/24.

Alisema serikali inapaswa kuanzisha mamlaka itakayosimamia sekta hizo kama ilivyofanyika katika kuanzisha Wakala wa Misitu Tanzania (TFS) na Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS) ambazo zinafanya kazi ya usimamizi majukumu ya wizara husika na kuongeza mapato.

Alisema kuwa na dira pia kutaisaidia wizara hiyo kuwa na mwelekeo unaoeleweka, kwamba kila waziri atakayeongoza atakuwa anajua anafanya nini na anatakiwa kufanya nini.

Gwajima alisema ni jambo lisilo na mashiko kwa sekta ya uvuvi kuchangia asilimia moja katika Pato la Taifa wakati nchi imezungukwa na maziwa katika mikoa mingi.

"Tanzania imezungukwa na maji, ukienda Lindi, Mtwara, Tanga, Pwani, Dar es Salaam yote imezungukwa na maji, Mwanza, Mara, Simiyu, Geita, Mbeya, Katavi, Rukwa, Kilimanjaro, Manyara kote huko kuna maziwa, halafu leo waziri anatueleza uvuvi imechangia asilimia moja kwenye Pato la Taifa. "Mikoa 21 imezungukwa na maji, haikubaliki wala haiingii akilini kwamba uvuvi ichangie asilimia moja katika Pato la Taifa. Tukitaka kuokoa hili ni lazima tuifanye sekta ya uvuvi iwe na mamlaka itakayosimamia baadhi ya majukumu," alisema.

Gwajima alisema Tanzania ina ng'ombe milioni 36.6, mbuzi milioni 26.6, kondoo milioni 9.1 lakini inaagiza maziwa kutoka nje ya nchi.

"Kwanini hizo fedha tulizopata faida tusizihifadhi, tuwe na dira ya uvuvi na mifugo ili kila waziri anayeingia kuiongoza wizara hiyo awe na mwelekeo utakaomwongoza?" Alihoji.

Hoja ya Gwajima iliungwa mkono na Mbunge wa Morogoro Kusini, Innocent Kalogeris, ambaye alisema kuundwa kwa mamlaka kutaisaidia wizara kupiga hatua kimaendeleo, kutatua kero na kuchangia zaidi katika Pato la Taifa. Alisema pia serikali inaweza kuanzisha mamlaka itakayokuwa chini ya wizara hiyo itakayokuwa na jukumu la kufanya shughuli za kuwasaidia wavuvi na wafugaji.

Alisema: "Kama tulivyoanzisha TARURA ikasaidia kutatua kero ya ukosefu wa barabara, REA ikasaidia upatikanaji wa umeme, hivyo hivyo tuanzishe wakala katika Wizara ya Uvuvi na Mifugo ili iende kutatua kero."



Mkurugenzi Mkuu Mamlaka ya Elimu Tanzania (TEA), Bahati Geuzye (kulia), akipokea cheti cha mshindi wa kwanza katika kundi la taasisi zinazojitegemea kutoka kwa Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Adolph Mkenda, wakati wa kilele cha Maadhimisho ya Wiki ya Ubunifu, jijini Dodoma mwishoni mwa wiki. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

## Benki yazindua tawi jipya kuwezesha fursa kiuchumi

**Na Joseph Mwendapole,** ARUSHA

BENKI ya Mwanga Hakika (MHB), imezindua tawi jipya na la kisasa jijini Arusha, ikiwa ni sehemu ya mkakati wa kutanua mtandao wake wa huduma za kifedha nchi nzima.

Tawi hilo jipya lililopo barabara ya Sokoine linafanya idadi ya matawi ya benki hiyo kufikia saba huku matawi mengine yakiwa Dar es Salaam, Moshi, Dodoma, Mwanga na Same.

Akizungumza wakati wa uzinduzi wa tawi hilo, Mkurugenzi Mtendaji wa benki hiyo, Jagjit Singh, alisema tawi hilo litarahisisha huduma kwa wateja wake na wakazi wa Arusha kwa ujumla.

"Tawi hili la hapa Arusha litarahisisha upatikanaji wa huduma za kifedha kwa kuwa lipo katikati ya jiji. Tawi ni la kisasa na lina sehemu maalum kwa ajili ya wateja wakubwa, vifaa vya kisasa na huduma ya kubadilisha fedha. Hii yote ni kuhakikisha kuwa wateja wetu wanapata huduma bora za kisasa na kwa urahisi," alisema.

Mkurugenzi huyo aliongeza kuwa tawi hilo limefunguliwa mahsusi kwa ajili ya fursa za kiuchumi zilizopo jijini Arusha ili ziwanufaishe wakazi wa jiji hilo.

"Tawi linalozinduliwa leo ni sehemu ya mkakati wetu wa kujitanua na kuwafikia wateja wengi zaidi. Lengo letu ni kuwafikia wateja popote pale walipo lakini tukizingatia utoaji wa huduma bora za kifedha zinazoendana na mahitaji yao," alifafanua.

Katika uzinduzi huo, Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Mwigulu Nchemba, alipongeza benki hiyo kwa kujikita katika kutoa huduma kwenye miradi ya miundombinu na kufanya kazi na wajasiriamali wadogo na wa kati.

"Ninapenda kuipongeza Benki ya Mwanga Hakika kwa jitihada zake za kujitanua na hivyo kutoa fursa za wananchi wa kada mbalimbali kufikiwa na huduma za kifedha pamoja na kusaidia sekta mbalimbali ikiwamo ujenzi wa miundombinu," alisema.

# Waziri: Maji ni sehemu ya maficho ukatili wa kijinsia

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Dk. Dorothy Gwajima, ametoa wito kwa mamlaka za maji kuongeza kasi ya usambazaji huduma ya maji kwa wananchi wengi zaidi ili kupunguza ukatili wa kijinsia na kuchochea usawa wa kijinsia.

Dk. Dorothy alitoa rai hiyo juzi alipotembelea banda la Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira (DAWASA), katika kilele cha tamasha la kutangaza fursa za maendeleo na kupinga ukatili wa kijinsia.

Tamasha hilo liliandaliwa na Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum katika Viwanja vya Leaders Club mkoani Dar es Salaam.

Waziri aliishukuru DAWASA kwa kuwa miongoni mwa washiriki katika tamasha hilo, akisema mapambano ya ukatili wa jinsia yanakwenda sanjari na upatikanaji wa huduma ya maji.

Alisema upatikanaji wa maji utawaepusha wanawake na watoto kutembea umbali mrefu kuyatafuta ambako hufanyiwa vitendo vya ukatili wa kijinsia njiani.

"Nimefurahi kuona DAWASA imeshiriki katika tamasha hili na tuendelee kushirikiana kwa sababu maji ni uhai na lazima tuwasogezee wananchi huduma ili wasihangaike kuyafuata umbali mrefu.

"Ukatili wa kijinsia unafanywa sana kwa makundi ya wanawake na watoto, tuongeze kasi ya upatikanaji huduma ili kuboresha maisha na ustawi wa jamii yetu," alisema waziri huyo.

Ofisa Mawasiliano wa DAWASA, Joseph Mkonyi, alisema mamlaka imefanikiwa kufikisha huduna ya maji ndani ya eneo lake la huduma kwa Mkoa wa Dar es Salaam na Pwani kwa asilimia 95 na hivyo kuisaidia serikali kuleta maendeleo na kukuza uchumi wa taifa.

"Mheshimiwa waziri, mamlaka imefanikiwa kutekeleza miradi ya maji maeneo mengi ya Mkoa wa Dar es Salaam, tunajivunia kukamilisha miradi mbambali inayoboresha maisha ya wananchi wetu.

"Mfano, maeneo mapya yaliyopata huduma kama vile Mivumoni, Goba, Madale, Makongo, Mshikamano, Pugu, Ukonga, Chalinze, Mkuranga na maeneo mengine mengi," alisema Mkonyi.





## Vifo wa watoto sasa vyapungua

**Na Jaliwason Jasson,** BABATI

SERIKALI imesema imefanikiwa kupunguza vifo vya watoto chini ya miaka mitano na wenye umri chini ya mwaka mmoja kwa asilimia 50, hasa kwa magonjwa ya ndui, polio, pepopunda na donda koo.

Mganga Mkuu wa Serikali, Prof. Tumaini Nagu, akizungumza na Nipashe kuhusu mafanikio hayo, alisema jambo hilo limewezekana kutokana na kutokomezwa magonjwa yanayozuilika kwa chanjo.

"Kitu kilichotusaidia kama taifa, kupunguza vifo vya watoto hao ni kutoa kipaumbele cha chanjo kwa watoto ili kuzuia magonjwa yanayozuilika kwa chanjo. Kulingana na rejea, chanjo husaidia kuzuia vifo milioni mbili mpaka milioni tatu duniani, kwa vifo vitokanavyo na maradhi yanayozuiliwa na chanjo duniani kote.

"Ingawa, bado kuna watoto ambao hawajakamilisha ratiba za chanjo, hasa ya surua na rubella. Tulianza kutoa hamasa kwa jamii kupeleka watoto kupata chanjo hiyo tangu Aprili 24 mpaka Aprili 30, mwaka huu nchini kote. Chanjo ya surua na rubella, inatolewa kwa mtoto akiwa na miezi tisa, na akiwa na mwaka mmoja na nusu," alisema.

Alipoulizwa kuhusu hali hiyo, Katibu Tawala wa Mkoa wa Manyara (RAS), Karolina Mtapula, alisema mkoa huo umetoa chanjo kwa asilimia 95 kwa mwaka jana.

Mtapula alisema kazi ya utoaji chanjo hiyo, imeendeshwa kwa mafanikio makubwa na wataalamu wa sekta ya afya.

# Miradi yabuniwa kukabili mabadiliko ya tabianchi

**Na Godfrey Mushi,** HAI

BAADA ya Shirika la Climate Action Network Tanzania (CAN Tanzania), kupunguza migogoro ya watumiaji maji inayosababishwa na mabadiliko ya tabianchi katika wilaya ya Hai mkoani Kilimanjaro, sasa limeahidi kuja na miradi mingine ya kukuza uchumi.

Kwa mujibu wa Mratibu wa Utafiti, Sera na Ubunifu wa CAN Tanzania, Mkombozi Mbekenga, miradi mipya itakayobuniwa na kutekelezwa wilayani hapa ni mahususi kwa ajili ya kuongeza uhimilivu katika kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi.

"Miradi yetu lengo lake ni kuiwezesha jamii na wakulima wadogo kukabiliana na umaskini, kupunguza uhaba wa chakula, kuleta usawa wa kijinsia na kupunguza migogoro ya watumia maji, inayosababishwa na mabadiliko ya tabianchi,"alisema.

Mbekenga pia alisema CAN Tanzania, mpaka kufikia sasa, imetekeleza mradi wa ujenzi wa visima viwili ambavyo vimekamilika. Kisima cha kijiji cha Mkombozi kina urefu wa mita 130 na kisima cha kijiji cha Kilimambogo kina urefu wa mita 80.

Pia CAN Tanzania imejenga bwawa moja katika kijiji cha Ngosero, lenye uwezo wa kubeba lita milioni 10, ambalo limejengwa na kukamilika na hadi sasa limekusanya maji ya mvua za vuli na mvua za masika. Kuhusu shughuli zitakazokabidhiwa kwa halmashauri ya wilaya hiyo na vijiji vya Kilimambogo, Ngosero na Mkombozi, bila uwapo wa fedha za mfadhili, Mbekenga aliwaomba wadau wa maendeleo, Halmashauri ya Wilaya ya Hai na jamii husika, kuongeza juhudi katika mbio zilizoanzishwa na mfadhili wao ambaye ni serikali ya Ujerumani, kupitia Shirika la GIZ.

Shughuli hizo ni pamoja na kujenga mifereji ya kusafirisha maji hadi kwenye mashamba yaliyoko mbali na visima, ulinzi wa eneo la mradi na mali zake, kupanda miti rafiki na majani juu ya bwawa na kukusanya ushuru kutoka kwa watumia maji. Nyingine ni kujenga uwezo kwa kamati za watumia maji na kujenga uwezo wa ziada kwa mafundi wa kuendesha mtambo wa nishati jadidifu.

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Hai, Edmund Rutaraka, akizungumzia miradi hiyo, alisema CAN Tanzania imeugusa moyo wwa wananchi wa Hai kupitia sekta ya umwagiliaji, ambayo itawasaidia kufikia azma yao ya kujitegemea kwa uzalishaji wa mazao mbalimbali na utunzaji mazingira.




Naibu Waziri wa Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu, Patrobas Katambi (kulia), akizungumza kuhusu udhibiti wa uhalifu wa mitandao, alipotembelea banda la Tigo, wakati wa maonyesho ya usalama na afya mahala pa kazi katika viwanja vya Tumbaku mkoani Morogoro mwishoni mwa wiki. Kushoto ni Meneja wa Kitengo cha Afya na Usalama wa Tigo, Dismas Anthony. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wanakijiji kunufaika na mradi wa nyuki

**Na Woinde Shizza,** ARUSHA

WAKAZI wa Kijiji cha Esilalei, Monduli mkoani Arusha, wataanza kunufaika kiuchumi kwa kurina asali na kuiuza katika soko la ndani na nje ya nchi, baada ya Hifadhi ya Taifa ya Ziwa Manyara kuanzisha na mradi wa ufugaji wa nyuki wa kisasa.

Hifadhi hiyo ya Taifa ya Ziwa Manyara, tayari imetoa mizinga 200 ya nyuki kwa wananchi hao kwa ajili ya kuwapiga jeki katika utunzaji wa mazingira na kujiongezea kipato.

Mkuu wa Wilaya hiyo, Joshua Nassari, alikabidhi jana mizinga hiyo huku akiipongeza Hifadhi ya Taifa ya Ziwa Manyara kwa kuja na mradi huo wa kuwawezesha wananchi kiuchumi.


"Nimeelezwa na Menejimenti ya Hifadhi ya Ziwa Manyara, kwamba mizinga yote ina thamani ya Sh. milioni 23. Tunatamani siku moja, tuwe na kiwanda kikubwa cha kuchakata asali hapa katika kijiji cha Esilalei, ambacho kitatoa ajira pia kwa watoto wenu," alisema.

Kwa sasa, Tanzania inatajwa kuwa sampuli za nyuki tofauti 223, ambao wanasaidia shughuli za uchavushaji.

Nassari alisema kwa kuwa asali ni biashara kubwa ndani ya nchi na nje ya nchi, ni vyema wakazi hao ambao wameunda vikundi vitano vya ufugaji wa nyuki, wakasimamia vizuri; na kuzingatia suala la vifungashio bora litakalosaidia soko lao kukua kwa haraka.

Kabla ya makabidhiano hayo, Kamishna Msaidizi wa Uhifadhi wa Hifadhi ya Taifa ya Ziwa Manyara, Neema Mollel, alisema idara ya uhusiano katika hifadhi hiyo inatumika kushirikiana kwa karibu na jamii, kwa kutoa elimu ya uhifadhi katika vijiji vyote vinavyozunguka hifadhi hiyo.

Pia alisema mradi huo umebuniwa mahususi katika kijiji hicho kutokana na uoto mzuri wa miti, ambao unawezesha nyuki kufika eneo hilo kwa urahisi na kuzalisha asali.





# Mwadui kuanza uchimbaji Agosti

**Na Marco Maduhu,** KISHAPU

MGODI wa uchimbaji almasi wa Wiliamson Diamond ulioko Mwadui, Kishapu mkoani Shinyanga, unatarajia kuanza rasmi tena uchimbaji madini Agosti, mwaka huu, baada ya kukamilika kwa ujenzi wa bwawa jipya.

Novemba 7, mwaka jana, bwawa linalohifadhi tope la mgodi huo, lilipasuka kingo zake kisha tope kuvamia makazi ya wananchi na kusababisha madhara makubwa, hali ambayo ilifanya mgodi huo kusitisha uchimbaji madini mpaka ujenzi wa bwawa jipya utakapokamilika.

Meneja Mkuu wa Mgodi huo, Mhandisi Ayoub Mwenda, alibainisha hayo juzi wakati Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, Christina Mndeme, alipofanya ziara kwenye mgodi huo kuona hatua za ujenzi wa bwawa hilo jipya.

Alisema ujenzi wa bwawa hilo umefikia asilimia 46 na litarajiwa kukamilika ifikapo Julai, mwaka huu, na kuwa tayari kwa kutumika na Agosti wanatarajia kuanza rasmi uchimbaji madini.

"Wakati tukiendelea kulitumia bwawa hilo pia tutaanza usanifu wa ujenzi wa bwawa lingine kubwa zaidi ya hili kuweka hali ya tahadhari na usalama kuepusha upasukaji kwa mara nyingine," alisema Mwenda.

Kuhusu ulipwaji fidia wananchi ambao waliathirika na bwawa hilo, alisema tayari wamelipa kwa asilimia 96 na ifikapo Juni, watawajengea nyumba wananchi 47 ambao nyumba zao ziliathiriwa zaidi na tope.

Mkuu wa Mkoa, Mndeme, aliutaka uongozi wa mgodi huo kuongeza kasi zaidi ya ujenzi wa bwawa hilo jipya na kulijenga kwa ubora unaotakiwa ili isitokee tena ajali na kusababisha athari kwa wananchi.

Alisisitiza kuwa bwawa hilo likianza kutumika, lifanyiwe ukaguzi mara kwa mara sambamba na matengenezo na kujifunza kutokana na makosa ya awali ili kusijetokea tena na lenyewe likapasuka na kuathiri wananchi ambao wanauzunguka mgodi huo.

Mndeme aliagiza pia kwa wananchi 47 ambao watajengewa nyumba zijengwe za kisasa na ubora wa hali ya juu, huku akiwaonya wananchi ambao wanauzunguka mgodi huo, kuacha pia tabia ya kuvamia eneo hilo la mwekezaji kwa ajili ya kuiba mchanga wa madini kwa kuwa ni kinyume cha sheria.

# RC ataka vigingi Serengeti viheshimiwe

**Na Timothy Itembe,** SERENGETI

MKUU wa Mkoa wa Mara, Selemani Mzee, amewataka wananchi wanaozunguka Hifadhi ya Taifa ya Serengeti (SENAPA) kuheshimu mawe ya mipaka yaliyowekwa na serikali ili kudhibiti migogoro na uvamizi katika hifadhi hiyo.

Alitoa agizo hilo juzi katika kijiji cha Gibaso wakati akifunga usimikaji wa vigingi uliokuwa ukiendelea kwa lengo la kubainisha mipaka ya hifadhi na wananchi wanaozunguka maeneo hayo.

"Licha ya shughuli hii kufanikiwa kwa asilimia 100 bado kuna baadhi ya watu hawakubaliani na uwekwaji wa vigingi hivi na kati yao wako baadhi ya madiwani lakini sasa sote tunatakiwa kungana na kuacha siasa katika suala hili na bikoni lazima ziheshimiwe," alisema Mzee.

Pia aliwapongeza baadhi ya viongozi waliofanikisha shughuli hiyo na kuwataka watu wa hifadhi ya Serengeti kushirikisha jamii inayowazunguka katika shughuli mbalimbali za kijamii ikiwa ni pamoja na kutekeleza miradi kwa mujibu wa sheria na kuwataka kuwachimbia mabwawa ya kunyweshea mifugo ili kuondokana na kero za mwingiliano hifadhini. Mkuu wa Hifadhi ya Serengeti, Izumbe Msindai, alisema wakati wa mchakato huo baadhi ya wananchi walifanikiwa kupata ajira ndogo ndogo za muda mfupi hali ambayo inaimarisha ushirikiano baina ya wananchi na wahifadhi.

Aliongeza kuwa atahakikisha watu wa hifadhi wanaendelea kutoa ushirikiano kwa jamii kupitia kitengo maalumu kilichoundwa hapo mwaka 1992 cha ujirani mwema ikiwa ni pamoja na kutekeleza miradi mbalimbali kwa jamii.

Pia alisema Sh. milioni 761 zimetengwa kwa ajili ya kutekeleza miradi ya kijamii ikiwamo kukarabati mabwawa mawili na kuchimba mengine mawili na jamii kutumia kunyweshea mifugo na matumizi mengine ya kijamii.

Ofisa Mpima Ardhi kutoka Wizara Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, John Sorwa, alisema uwekwaji mawe hayo kutenganisha mipaka ya hifadhi na wananchi, umetekelezwa na kumalizika vizuri pia kwa ushirikiano wa wananchi.



Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, Christina Mndeme (wa pili kulia), akikagua ujenzi wa bwawa jipya la kuhifadhia majitope katika Mgodi wa Almasi wa Williamson Diamond, Mwadui, wilayani Kishapu mkoani humo juzi, baada ya bwawa la awali kupasuka kingo zake Novemba mwaka jana na tope kuvamia makazi ya watu na kuleta madhara makubwa. Bwawa hilo jipya linatarajia kukamilika Julai mwaka huu. **PICHA: MARCO MADUH**U

# Wazee 5,200 wapewa bima za afya bure

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

HALMASHAURI ya Manispaa ya Kahama mkoani Shinyanga, imetoa bima za afya za CHF iliyoboreshwa bure kwa wazee 5,210 kutoka kata 20 za halmashauri hiyo ili kuwarahisishia upatikanaji wa huduma za matibabu katika hospitali na vituo vya afya, zenye thamani ya Sh. milioni 38.2 kutoka fedha za mapato ya ndani.

Katibu wa Baraza la Wazee Taifa, Anderson Lyimo, alisema hayo juzi wakati akitoa taarifa ya upatikanaji wa bima za afya kwa wazee katika kikao cha kawaida cha baraza la madiwani cha robo ya tatu ya mwaka wa fedha 2022/23. Alisema kila mzee asiye na uwezo, ana sifa ya kupata bima ya afya bila masharti.

Alisema halmashauri hiyo imekuwa ikitenga fedha kila mwaka kwa ajili ya kuwakatia bima za afya ya CHF iliyoboreshwa wazee na kuzihuisha na tangu mwaka 2017 mpaka sasa, wazee wapatao 5,210 wamepatiwa bima hizo ambazo zinawarahisishia kupata matibabu bure katika zahanati, vituo vya afya na hospitali.

Aidha, Lyimo alisema katika robo hii ya tatu ya mwaka wa fedha 2022/23, halmashauri pia imetenga Sh. milioni sita za kuwakatia bima ya afya wazee 1,200 sawa na wastani wa wazee 60 kila kata 20 wasio na uwezo na kuwataka wadau kujitokeza na kusaidia kundi hilo kama walivyofanya Kanisa la Mito ya Baraka kutoa bima kwa wazee 70.

"Manispaa hii ina jumla ya wazee 6,692 baadhi yao wana bima za Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF) na wengine za CHF iliyoboreshwa. Kila mwaka wa fedha tumekuwa tukiwakatia bima na kuzihuhisha zile zilizokwisha muda. Tumekuwa tukisaidiana pia na madhehebu ya kidini na hivi karibuni kanisa la Mito ya Baraka lilitoka bima kwa wazee 70," alisema.

Mbunge wa Kahama, Jumanne Kishimba, alisema mikoa ya Kanda ya Ziwa inaongoza kwa ukatili wa wazee yakiwamo mauaji kwa imani za kishirikina, hivyo inatakiwa kuanzishwa kwa vituo vya kulelea wazee kama ilivyo vituo vya kulea watoto yatima na itasaidia wazee kupata mahitaji yao na kuondokana na ombaomba mitaani.

Naye Mwenyekiti wa CCM Wilaya ya Kahama, Thomas Muyonga, aliwataka madiwani kupitia mikutano ya hadhara wanayoifanya kuwakumbusha wananchi juu ya maadili ikiwamo kuwalea wazee wao nasio kuwatelekeza na kuanza kurandaranda mitaani, serikali imekuwa ikitenga fedha nyingi kila mwaka kwa ajili yao na huku wapo wa kuwalea.

# ama

ALHAMISI MEI 4, 2023

AFYA NA MAZINGIRA




Ukurasa 12

**Mkoa Geita waingia ubia na wachimbaji wakubwa kufukia mashimo, kupanda miti**



Ukurasa 13

Kituo cha kwanza afya macho, tangu mkoa Katavi kuanzishwa miaka 11



Ukurasa 14

**NEMC yaja na meno kamili kutafuna wabishi wanaopiga kelele mitaani**

AFYA

# Operesheni ya Rais Samia, mradi maji kufika malengo iko bayana

• Kufika 85.06%, Waziri Makamba amrejeshea asante

**Na Maulid Mmbaga,** ALIYEKUWA RUFIJI



Ndivyo lilivyo Bwawa la Umeme Julius Nyerere. **PICHA: MTANDAO**

WAKATI anachukua uongozi nchini, Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, mbali na mikakati mipya, alinua kuendeleza aliyoachiwa na mtangulizi wake, marehemu Dk. John Magufuli. Hapo kunatajwa miradi miwili mikubwa, ujenzi wa reli ya kisasa, SGR na Bwawa la Umeme la Julius Nyerere.

Ni mradi ulioko katika Hifadhi ya Selous wilayani Rufiji, mkoa wa Pwani, unaandaliwa kuwezesha utoaji umeme mkubwa nchini na mpaka sasa, maendeleo ya ujenzi yanatajwa kufika asilimia 85.06 chini ya Rais Dk. Samia, kutoka asilimia 37 alizopokea mtangulizi wake, Dk. John Pombe Magufuli.

Waziri wa Nishati, January Makamba, anaiambia Nipashe, kuwa zimebaki mita za ujazo 13, kufikia 163 kutoka usawa wa bahari, bwawa lianze kuzalisha umeme na hadi sasa maji yamefikia mita za ujazo 150, akipataja ni penye matumaini.

"Pia, linatarajiwa kuwa na lita za ujazo bilioni 30 na mpaka sasa ambazo tayari zimeshajaa ni bilioni sita sawa na asilimia 20 tangu kuanza kujaza maji," anasema Waziri Makamba, anayetumia takwimu kutathmini kiwango cha maji yaliyoingia wiki mbili zilizopita ni mengi kuliko yaliyoleta mafuriko nyuma 2019/2020, ikiashiria ujenzi wa tuta unadhibiti mafuriko kwa asilimia kubwa.

Hadi sasa mradi una thamani ya shilingi trilioni 6.5, ukitarajiwa kuchangia uzalishaji umeme megawati 2,115, hata kuondoa adha ya mgawo wa umeme nchini.

Wakati hitaji la umeme kitaifa likitajwa kuwa megawati 2000, Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) linazalisha megawati 1,601 na matarajio ya mradi utakapokamilika na kuanza kazi, utazalisha megawati 3,716.

"Sisi watu wa wizara (Nishati) kwa kushirikiana na kila mmoja wetu, tunaona fahari kubwa kuona sasa ujazaji wa maji umefikia mita za ujazo (cubic meters) bilioni sita. Haya ni mafanikio makubwa kwa serikali na Rais wetu (Dk. Samia) kwa sababu nguvu yake aliyoweka na jinsi anavyoyotusimamia, imesababisha mradi wote kwa ujumla kufikia asilimia 86, kutoka asilimia 37 alizokuta wakati anapewa madaraka," anasema Makamba.

Pia, anaeleza binafsi kuridhishwa na kazi ya mkandarasi wa mradi, akisema zimebakia mita 13 za ujazo kwa mitambo ya kufua umeme ianze kuzungushwa na maji kuzalisha umeme.

Kiwango hicho anakitaja kimepita matarajio na malengo ya Rais Dk. Samia aliyoweka, wakati anaenda kushuhudia ujazaji maji bwawa hilo kwa mara ya kwanza, kati ya Desemba 2021 na mwaka 2022.

Anataja ujenzi wa matuta eneo la mradi wenye thamani ya shilingi trilioni 6.5, umeleta ahueni kudhibiti mafuriko jirani yaliyoshuhudiwa. Matarajio ni kuzalishwa umeme megawati 2,115.

Kimsingi, taifa lina uhitaji wa umeme megawati 2,000, huku likizalisha umeme megawati 1,601, matarajio ni kuwapo megawati 3,716, pale utakapomilika kuanza kazi kama inavyokusudiwa.

Wakati Rais Dk. Samia alipotembelea Bwawa la Mwalimu Nyerere, akaonyesha shauku kuona serikali inafanikisha wazo lililoanza tangu zama za Mwalimu Julius Nyerere, akiwa madarakani.

"Nchi yetu chini ya uongozi wa hayati Dk. John Pombe Magufuli katika awamu ya tano, tulisema liwalo na liwe, lakini wazo la mradi huu lazima tulifanikishe kwa vitendo kwa sababu tunajua utatuletea umeme wa uhakika na endelevu.

"Mradi huu utaimarisha na kufungua fursa nyingi za utalii katika eneo la Kusini mwa Tanzania, hususani katika Hifadhi ya Taifa ya Nyerere, hivyo kutoa ajira moja kwa moja na nyinginezo," anatamka Rais Dk. Samia, ambaye akaanza kushughulikia mradi huo katika tafsiri ya kimkakati, akiweka nguvu kubwa kufanikisha kwa wazo la waasisi wa nchi.

Kwa mujibu wa Waziri Makamba, mradi huo unachukua asilimia tatu ya sehemu hiyo ya hifadhi ya wanyama, yenye ukubwa wa kilomita za mraba 50,000.

**MANUFAA YAJITOKEZA**

Waziri Makamba ana ufafanuzi ziarani wiki iliyopita, akasema mradi JNHPP kwa kiasi kikubwa umezuia mafuriko kwa wakazi wanaoishi jirani, mikoa ya Pwani na Morogoro hasa kipindi cha mvua.

**INAENDELEA UK.12**

MAZINGIRA

## BAADA YA ATHARI ZA WACHIMBAJI WADOGO...

# Mkoa Geita waingia ubia na wachimbaji wakubwa kufukia mashimo, kupanda miti

**Na Marco Maduhu** ALIYEKUWA GEITA




Shughuli zikiendelea za kufukia mashimo yatokanayo na uchimbaji madini holela katika mgodi wa Nyamatagata, Geita. **PICHA: MARCO MADUHU**

WACHIMBAJI wadogo wa madini, ikiwamo dhahabu, sifa moja yao kuu inatajwa wanaharibu mazingira wawapo kazini, kwa sababu hawana vifaa maalumu kubaini uwapo wa madini katika eneo husika, hivyo wanachimba kwa kubashiri, hata wanaacha mashimo.

Ni hali inayotajwa kuchangia kuachwa mashimo, huku wakikata miti muhimu kwa kutunza mazingira. Katika kata ya Mgusu, Halmashauri ya Geita Mji, machimbo ya Nyamatagata, yaliyoanza Mei 20, mwaka jana, wachimbaji baada ya kusikia kuna madini, wanaelezwa wakapavamia na kuanza shughuli za uchimbaji, hata kusababisha uharibifu mkubwa wa mazingira.

Ofisa Mazingira wa Halmashauri ya Geita Mji, Bingile Washima, anasema serikali kwa kushirikiana na wadau mbalimbali, ikiwamo Timu ya Wanasheria Watetezi wa Mazingira kwa Vitendo (LEAT), anasema wamekuwa wakijitahidi kuwapa elimu wachimbaji wadogo wachimbe bila ya kuathiri mazingira.

Tito Mlelwa, ni Ofisa Mazingira Mkoa wa Geita, anasema kwa kawaida wachimbaji wadogo wanafahamika kuwa waharibifu wa mazingira, lakini kwa machimbo ya Nyamatagata, kupitia wamiliki wa leseni, wamebadili mwenendo kurejea utunzaji mazingira, ikianza na elimu sahihi kwa jamii husika.

Katika hilo, Ofisa Mtendaji wa Mtaa wa Manga, Kata ya Mgusu, ndani ya Halmashauri ya Geita Mji, Boniphace James, anasema eneo ambalo shughuli za uchimbaji madini zinafanyika katika Machimbo ya Nyamatagata, kuna marufuku kwa mchimbaji kukata miti na hata miti inayotumika hapo sasa, inatoka maeneo mengine ya nchi, ikiwamo Bukoba, Tarime na Mbeya.

Anasema katika utunzaji mazingira mgodini, viongozi wanaoshirikiana na kampuni yenye leseni kama, Geita Resources, wanafukia mashimo maeneo yote ya ardhi, ambako kumeathiriwa, wakipanda miti, ikiwa ni jukumu endelevu, kuzuia uharibifu wa mazingira katika machimbo hayo.

Kamanda wa jeshi la jadi Sungusungu katika machimbo hayo, Mathias Mwita, anasema wamekuwa wakifanya doria za kila mara kudhibiti uharibifu wa mazingira, ikiwamo ukataji miti na wanaofanya makosa huchukuliwa za kisheria.

"Watu ambao tunawakamata wakichafua mazingira huwa tunawatoza faini kuanzia shilingi 2,000 hadi 5,000, wale wanaokata miti faini zao zipo juu kuanzia shilingi 50,000 na kuendelea," anasema Kamanda huyo Sungusungu.

Ofisa Mtendaji wa Kata ya Mgusu, Halmashauri ya Geita Mji, Elias Galila, anasema wakati machimbo hayo yanaanza mwaka jana, hali mahali hapo ilikuwa mbaya, kwa sababu ya kuwapo idadi kubwa ya wakazi, wastani tu 20,000.

Anaeleza hatua walizochukua ni kuwakamisha jukumu la kufukia mashimo wamiliki wa leseni, ikiwamo kampuni ya Geita Resources, pia wakapanda miti maeneo hayo, huku viongozi wa eneo hilo wakitumia sheria za usimamizi mazingira kupadhibiti.

"Kihistoria eneo hilo lilikuwa na miti sana ya asili, lakini baada ya shughuli za uchimbaji madini kuanza, miti ya asili ilikatwa, na sisi tumewekeana sheria zetu marufuku kukata miti ambayo imesalia, bali wachimbaji wanunue miti kutoka maeneo mengine," anasema Kamanda wa Sungusungu, Mwita.

**UONGOZI MKOA**

Mkuu wa Wilaya ya Geita, Cornel Magembe, anasema asilimia 70 ya wananchi mkoani Geita wanajishughulisha na uchimbaji madini na anataka uchimbaji huo uendane na utunzaji mazingira kwa mujibu wa Sheria ya Madini ya Mwaka 2010 na Sheria ya Mazingira ya Mwaka 2004, ambazo zinasisitiza utunzaji mazingira.

"Tunataka uchimbaji wa nadini hapa Geita uendane sambamba na utunzaji wa nazingira, wachimbaji wakichimba madini wasiache mashimo ovyo wayafukie hii ni kwa faida ya vizazi vijavyo," anasema Magembe.

Kaimu Ofisa Madini Mkazi Mkoa wa Geita, Mhandisi Martin Shija, anawakumbusha wachimbaji wadogo wa madini, wanapaswa kutekeleza mpango wa utunzaji mazingira kwa mujibu wa sheria na wasiotekeleza, sheria ziko wazi, ikiwamo kunyang'anywa leseni za uchimbaji, kwa sababu wanakuwa wamekiuka mpango huo.

**INAENDELEA UK.14**

# Operesheni ya Rais Samia, mradi maji kufika malengo iko bayana

**INATOKA UK.11**

"Tunafurahi kwamba tayari tumefikia mojawapo ya malengo makubwa ya kuanzishwa kwa mradi huu, ikiwamo kuwakinga wananchi na madhara yatokanayo na mafuriko," anasema.

Vilevile, waziri anaeleza kiasi maji ya mvua kilichoingia kwenye bwawa mwezi Aprili mwaka huu, kinafanana na cha mvua zilizonyesha kati ya Desemba 2019 hadi 2020, hata kusababisha mafuriko katika mikoa hiyo miwili.

"Kwa mvua hizi zilizonyesha katika kipindi cha wiki mbili zilizopita na hasa siku hizi mbili hadi kufikia leo, tungesikia taarifa za vifo na uharibifu, lakini kutokana na mradi huu, jambo hilo halijatokea mwaka huu...

"Wakati Rais Samia Suluhu Hassan anachukua madaraka, ujenzi ulikuwa asilimia 37, mradi ameenda nao ametoa pesa, ametusimamia na ametuhimiza na sisi tumesimamia walio chini yetu na wao wamesimamia wa chini yao na kufanikisha kuwapo hapa tulipo leo," anasema Makamba.

Hapo, pia anaelekezea pongezi TANESCO, akiwasifu wafanyakazi wale kushirikiana na Mhandisi Mkazi, Lusajo Mwandambo, wanaohakikisha kazi inafanyika usiku na mchana.

Mkurugenzi Mtendaji wa TANESCO, Maharage Chande, anamwahidi Waziri, mradi kukamilika kwa wakati, ili kupunguza kero ya ukosefu wa umeme nchini.

"Mtanzania yeyote, kushiriki ujenzi wa mradi huu," anasema na kuongeza: "Wito wangu kwa wafanyakazi wenzangu wa TANESCO ni kwamba, tusianze kuzembea kwa sababu tunaona kazi inakaribia kumalizika, huu ndio wakati wa kuchapa kazi bila kuchoka."

Mhandisi Mkazi wa Mradi, Lutengano Mwandambo, anasema wanaanza kujaza maji bwawa hilo litakalokuwa na uwezo mkubwa kuzalisha umeme, akitaja kiwango kinachotakiwa kujaa katika bwawa hilo ni mita 184 kutoka usawa wa bahari.

Kwa sasa anataja kazi zinazoendelea katika mradi, ni usimikaji mageti saba katika njia zitakazoruhusu maji yanapokuwa mengi na kuzidi kiwango cha juu mita 190 kutoka usawa wa bahari.

Anasema ujenzi wa tuta kuu unaenda sambamba na mahandaki matatu ya kupitisha maji, ambayo ujenzi wake umefikia asilimia 98.47 hadi kufikia Februari 28, mwaka huu.

**MHANDISI MKAZI**

Mhandisi Mwamdambo anataja kingo nne za kuzuia maji zenye urefu wa kilomita 17.4, ambazo kazi yake ni kuzuia maji yasitoke eneo lake, akiendelea: "Ujenzi wa bwawa la JNHPP unaenda sambamba na ujenzi wa kituo kikubwa cha kupokea, kupoza na kusambaza umeme mkubwa kilichoko Chalinze, kituo hicho kitapokea umeme mkubwa wa kilovoti 400 kutoka katika mradi huu.

"Kituo hicho kitapooza hadi kufikia kilovolti 132 na kuuingiza kwenye gridi ya Taifa, tayari kusambaza katika kituo cha Kinyerezi Dar es Salaam, Tanga na Dodoma, pia tayari transfoma kubwa sita zenye uwezo wa megavolti 250 kila moja zimeshawasili eneo la mradi."

Anafafanua kuhusu transfoma hizo sita, nne ni za kupoza umeme mkubwa wa kilovolti 400 hadi 220 na mbili, zina uwezo wa kupoza umeme kilovolti 220 hadi 132.

"TANESCO inaishukuru serikali inayoongozwa na Rais Samia kwa jitihada za kuwezesha kufikia hatua ya kuanza kujaza maji ndani ya bwawa la Julius Nyerere na kuendelea kutoa fedha za mradi huu," anahitimisha Waziri Makamba.

• Taarifa hii ni baada ya mwandishi kuzuru hapo. Hivi karibuni.

AFYA

# Kituo cha kwanza afya macho, tangu mkoa Katavi kuanzishwa miaka 11

**Na Neema Hussein,** MPANDA

MKOA wa Katavi unatajwa hauna kituo cha huduma za matibabu ya macho tangu kuanzishwa miaka 11 sasa, hatua inayosbabisha huduma hiyo kwa baadhi ya wagonjwa wakubwa, ipatikane kwa gharama kubwa.

Sasa hatua imechukuliwa, kwa Mkuu wa Mkoa, Mwanamvua Mrindoko, kazindua kituo cha kwanza kitakachotoa huduma kimkoa kinachoitwa

Mtakatifu Aloyce, chini ya Shirika la Tanzan Eye kutoka nchini Ujerumani, chini ya Kanisa la Katoliki Jimbo la Mpanda, kitakachotoa huduma, matarajio ni kwamba itapunguza gharama za matibabu wakazi 192,000 waliokutwa na matatizo mbalimbali ya macho kwa mwaka 2022.

Mganga Mkuu wa Mkoa, Jonathan Budenu, anasema kituo hicho kimekuja katika wakati sahihi kulingana na mahitaji makubwa ya huduma za matibabu, akifafanua idadi hiyo ya wagonjwa wa macho ni sawa na asilimia moja ya wakazi wote mkoani Katavi, wengi walipewa rufani kwenda nje ya mkoa.

"Tatizo hilo la macho kwa mkoa wa Katavi sio dogo, ni kubwa na linahitaji kuwa na maeneo mahususi na nyie mmekuwa wa kwanza kuwa na eneo hili, mahususi la utoaji huduma za macho niwapongeze sana.

"Nawaomba wananchi watumie kituo hiki kuja kufanya 'check up' na kujua afya ya macho inavyoendelea, ili kuweza kupata huduma stahiki, mapema na kuhakikisha afya ya macho haiteterek.

"Mimi pia nikiwa mdau mkubwa wa jengo hili, ninaamini kabisa sisi wote ambao ni wagonjwa wa macho, basi tutapata huduma bora na wale waliokabidhiwa kutoa huduma hapa walitunze jengo, vifaa ikiwa ni pamoja na kutoa huduma iliyotukuka," anatamka.

Mkuu wa Mkoa anaendelea:"Kama kubadilisha miwani, basi haitahitajika mimi kupanda gari au ndege au usafiri wowote kwenda Dodoma au Dar es Salaam kufuata huduma za miwani, tutazipata hapa, mimi na wananchi wangu wa mkoa wa Katavi."

"Tunashukuru sana kwa sababu mmeokoa gharama kubwa ya kifedha, kiuchumi na muda, ambao tungeweza kutumia kwenda kutafuta huduma za macho mikoa mingine," Mrindoko anaendelea, akiunganisha pongezi zake kwa kanisa hilo, pia inayofanya katika elimu na ujasiriamali, akiahidi serikali ya mkoa iitendelea kuwaunga mkono.

"Nitoe wito tu, jengo hilo ni jipya, kubwa na zuri. Mara baada ya vifaa kufika hapa Mpanda, huduma zitatolewa mara moja. Niendelee kusisitiza Ofisi ya Mganga Mkuu wa Mkoa na sekta ya afya wilaya zote kuunga mkono na kushirikiana vizuri kutoa utaalamu wenu, kuhakikisha huduma hapa ya macho inatolewa kwa ufanisi mkubwa katika eneo hili.

"Niwaombe na wadau wengine ndani ya Tanzania na nje kuendelea kuunga mkono jitihada za serikali katika utoaji huduma, kwa kuja kuwekeza miundombinu mbalimbali ya utoaji huduma, kama vile huduma za afya, elimu, maji, barabara na nyinginezo ambazo, bado kutokana na upya wa mkoa wetu huduma hizo, bado zinahitajika sana ndani ya mkoa wetu wa Katavi.

"Kwa hiyo, niwakaribishe sana na niwahakikishie mtakapofika katika kufanya uwekezaji huo wa kiuchumi na huduma, sisi serikali tutawaunga mkono, tutawasaidia, tutashirikiana nao kuhakikisha wanafanikiwa na sisi tunafanikiwa, katika kuwafikia wananchi wa mkoa Katavi," anaahidi Mrindoko.



Mkuu wa Mkoa Katavi, Mwanamvua Mrindoko (katikati aliyekaa), akiwa na viongozi wa hospitali hiyo, pia Kanisa Katoliki Jimbo la Mpanda, linaloimiliki. **PICHA ZOTE: NEEMA HUSSEIN**



Jengo la hospitali mpya ya macho wilayani Mpanda, mkoani Katavi.

**WENYE MRADI**

Mwakilishi Mkazi kutoka Shirika la Tanzan Eye, Ryner Linuma, katika taarifa yake anasema shirika lilianza kazi mkoani Rukwa na baada ya kuona kuna uhitaji katika mikoa mingine, wakaanzisha huduma katika mikoa ya Katavi na Kigoma.

Anasema, shughuli zinazofanywa na shirika hilo Katavi, zinajumuisha kugharamia masomo kwa wataalamu wa macho 16 wanaotambulika kama wauguzi wasaidizi wa macho, sasa wakifanya kazi katika hospitali zote za halmashauri mkoa wa Katavi na vituo vingine vya afya.

"Shirika pia limekuwa likitoa huduma za macho kwa njia ya mkoba, kuanzia Julai 2021, ilikuwa ikitolewa mara mbili kwa mwaka, ikihusisha madaktari bingwa na wabobezi kutoka Ujerumani na wataalamu wengine kutoka mkoani Katavi.

"Zaidi ya watu 3,692 waliokuwa na matatizo mbalimbali ya macho wamepatiwa huduma, kati yao 990 walifanyiwa upasuaji wa mtoto wa jicho, 295 walikuwa na uhitaji wa miwani, watu 196 walipatiwa miwani na wale ambao walihitaji huduma maalumu za upasuaji, walipatiwa rufani kwenda hospitali ya KCMC Moshi na Hospitali ya Taifa Muhimbili.

"Wagonjwa wengi waliohudumiwa walitoka halmashauri za mkoa wa Katavi na wengine walitoka Kigoma na Tabora hususani Halmashauri ya Kaliua. Baada ya kuona uhitaji ni mkubwa zaidi, shirika liliona kuwa na kambi mara mbili kwa mwaka haitoshi, hivyo tulikubaliana kwa pamoja kuanzisha programu maalumu ya kuzuia upofu unaoweza kuzuilika katika mikoa ya magharibi ya Tanzania," anasema.

Kwa mujibu wa Ryner, kupitia huduma jumuishi za macho wanazotoa katika mikoa ya Rukwa, Katavi na Kigoma, ina malengo ya kusomesha wataalamu wazawa katika ubobezi wa huduma za macho, kuboresha miundombinu kwa kujenga kituo maalumu cha matibabu kwa mikoa hiyo na kutoa vifaa tiba.

"Mafanikio yaliyopatikana ni kusomesha wauguzi 21 katika fani ya macho, kumpata daktari mmoja bingwa wa upasuaji wa mtoto wa jicho, ambaye ameazimwa kutoka Sumbawanga. Tumefanikiwa kusomesha pia wataalamu wa miwani ambao bado wapo masomoni, kutoa vifaa tiba katika kituo hiki na vingine vya mkoa wa Katavi," anasema Ryner, anayedokeza, pia mafanikio ya kupata jengo hilo la wagonjwa wa nje na upasuaji wa macho.

Anasema jengo hilo limeanza kujengwa Juni 2022, likigharimu Sh. bilioni 1.090 pamoja na vifaa vyenye thamani shilingi milioni 658, kukijengwa jengo na uboreshaji mazingira ya nje, kwa thamani shilingi milioni 332 na ununuzi wa vifaa tiba na visivyotiba.

Askofu wa Jimbo la Katoliki la Mpanda, Eusebius Nzigilwa, anatoa maagizo kwa watumishi wa kituo hicho kulitunza jengo hilo pamoja na vifaa vyake, ikijumuisha kuzingatia maadili, weledi kitaalamu na tabia za kiimani, ili kuwahudumia kwa ufanisi kibinadamu wahitaji wanaofika kupata huduma za macho.

Mkurugenzi wa Mradi huo wa Macho kituoni hapo, Dk. Karsten Paust, anataja huduma zitakazotolewa zinamlenga kila mhitaji, hasa wa mkoa wa Katavi na mingine jirani.

Tukio hilo la uzinduzi huo, limeambatana na la utunzaji wa mazingira, ambao Mkuu wa Mkoa Mrindoko, Askofu Jimbo Katoliki la Mpanda, Eusebius Nzigilwa na Mkurugenzi Dk. Karsten Paust, wamepanda mti kama kumbukumbu katika eneo hilo.

> **Nawaomba wananchi watumie kituo hiki kuja kufanya 'check up' na kujua afya ya macho inavyoendelea, ili kuweza kupata huduma stahiki, mapema na kuhakikisha afya ya macho haiteterek.**

MAZINGIRA

# NEMC yaja na meno kamili kutafuna wabishi wanaopiga kelele mitaani

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

HIVI karibuni Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC), lilitangaza mwezi huu linaanza operesheni kudhibiti kelele, ili kulinda afya za wananchi.

Mkurugenzi Mkuu wa NEMC, Dk. Samuel Gwamaka, anasema afya za watu wengi zinaathirika kwa kelele chafuzi zinazotokana na vyanzo mbalimbali.

Anatoa tafsiri ya Sheria ya Mazingira 2004, kwamba:"Kelele ni kila uchafuzi usababishwao na sauti ambayo kwa asili inakataliwa au ile iwezayo kusababisha athari mbaya kwa afya ya binadamu, maisha au mazingira; pia ni pamoja na sauti iwezayo kubainishwa na Kamati ya Taifa ya Viwango vya Mazingira."

Dk. Gwamaka anazitaja kuwa shughuli za kibinadamu zinasababisha kelele chafuzi na mitetemo, utafiti ukionyesha vyanzo vyake unajumuisha mitetemo, pamoja na ujenzi, nyumba au kumbi za starehe, viwanda, nyumba za ibada, vyombo vya usafiri na magari ya matangazo.

Anaeleza athari za wazi za ni kuhatarisha afya, mfano kukosesha wagonjwa muda wa kupumzika au wanafunzi muda wanapokosa muda wa kusoma, pia inaharibu mahusiano ya kijamii.



Mkurugenzi Mkuu wa NEMC, Dk. Samuel Gwamaka. **PICHA: MAKTABA**

### NAMNA YA KUZUIA

Meneja wa Ufuatiliaji wa Sheria wa NEMC, Ndimbumi Joramu, anatamka kifungu cha Sheria ya Mazingira, 2004: "Si ruhusa kwa mtu yeyote kupiga kelele au kusababisha kupiga kelele kuzidi kiwango kilichoainishwa au kitakachobainishwa kuhusiana na upigaji kelele... Litakuwa ni kosa kwa mtu yeyote kumwaga uchafu au kupiga kelele bila kuzingatia njia iliyobainishwa kuwa ni bora katika kanuni zinazoweza kutungwa na waziri."

Anasema katika kudhibiti kelele chafuzi, waziri mwenye dhamana ya mazingira kupitia Sheria ya Usimamizi wa Mazingira, ametunga Kanuni za Usimamizi wa Mazingira za Viwango vya Udhibiti wa Kelele na Mitetemo za Mwaka 2015.

Joramu anasema, NEMC inanuia kuhakikisha ulinzi wa afya ya binadamu na mazingira kwa kudhibiti viwango vya kelele na mitetemo kutoka vyanzo mbalimbali. Anafafanua hatua zingine: "Kubainisha viwango vya juu vya kelele vinavyoruhusiwa kutoka katika shughuli mbalimbali, kuweka udhibiti wa kelele na mitetemo na namna bora ya kuzuia athari zinazoweza kujitokeza."

### VIWANGO VINAVYORUHUSIWA

Mwanasheria huyo anataja kanuni za viwango vya kelele na mitetemo vilivyoruhusiwa na vinavyoweza kuvumilika kwa nyakati za mchana na usiku kwamba: "Viwango vya sauti vilivyoruhusiwa katika maeneo ya burudani, nyakati za mchana zinaanzia saa 12.00 asubuhi hadi saa 4.00 usiku. Viwango vya sauti vilivyoruhusiwa ni desibeli 60 katika makazi ya watu, 75 katika maeneo ya biashara na 85 katika maeneo ya viwanda."

Pia, anasema kuanzia saa 4.00 usiku hadi saa 12.00 asubuhi, viwango vya sauti vilivyoruhusiwa kwa nyakati hizo ni desibeli 40 katika makazi ya watu, 50 katika maeneo ya biashara na 65 viwandani.

Mkurugenzi wa Uzingatiaji na Utekelezaji wa Sheria ya Mazingira NEMC, Mhandisi Redempta Samuel, anataja kanuni inayotoa katazo la ujumla dhidi ya kelele chafunzi kwa yoyote hataruhusiwa kupiga au kusababisha kelele zilizo kubwa na zisizo na ulazima, au zisizo za kawaida na zinakera, kuleta usumbufu au kusababisha madhara katika afya na usalama wa watu ama mazingira.

"Kanuni ya 7(2) imeainisha mambo muhimu ya kuzingatia ili kujua au kupima kama sauti inayotoka imezidi au haijazidi kiwango kinachotakiwa; mambo hayo ni pamoja na muda (mchana au usiku), ukaribu na makazi ya watu, na ukaribu na hospitali au shule," anasema.

Hata hivyo, anasema wajibu wa mmiliki wa miundombinu wanaelekezwa na kanuni husika, wajibu wa mmiliki wa miundombinu au mtambo, ikiwamo vifaa vya muziki wanapaswa kuwa na kifaa cha kupima sauti, ambacho kinafaa kuwekwa katika miundombinu na ni kosa la kisheria kutokuwa nacho.

Pia, kunatajwa mamlaka za serikali za mitaa zina wajibu wa kusimamia utekelezaji Sheria ya Mazingira na kwa mujibu wa kanuni iliyopo, maofisa mazingira katika serikali za mitaa wamepewa mamlaka kutoa amri za utekelezaji kwa mhusika yeyote.

Mkurugenzi huyo anasema, NEMC ina nafasi ya kuwatumia wakaguzi wa mazingira na maofisa mazingira katika halmashauri zote, kuwa na mamlaka ya kusimamia kanuni au kutoa amri mbalimbali, zikiwamo za kumzuia mtumiaji mtambo wa kutoa sauti inayokiuka viwango vilivyoainishwa.

### FAINI NA ADHABU

Redemta anataja mamlaka ya NEMC, inaweza kumuamuru mkosaji kulipa faini ya fedha kisheria kwa kosa alilolitenda chini ya kanuni zilizopo kisheria. Anafafanua: "Mtu yeyote atakayekiuka matakwa ya kanuni hizi, anaweza kutozwa faini isiyopungua shilingi milioni mbili na isiyozidi shilingi milioni kumi au kifungo cha miaka miwili jela na kisichozidi miaka saba au vyote kwa pamoja."

Anasema, NEMC imebaini tatizo la baadhi ya wamiliki kutokuwa na kifaa cha kupima kiwango cha sauti inayotoka, uelewa hafifu juu ya madhara yatokanayo na sauti na mitetemo, hata hawana ushirikiano mzuri na mamlaka nyingine zinazosimamia utekelezaji sheria.

## Mkoa Geita waingia ubia na wachimbaji wakubwa kufukia mashimo

**INATOKA UK.12**

### WENYE MGODI

Meneja wa Kampuni ya Mgodi wa Stamico Gold Mining Operative Society uliopo Nyarugusu wilayani Geita, Hoja Shikome, anakiri wachimbaji wadogo wanaharibu mazingira, akitaja sababu, hawana vifaa maalumu vya kubaini madini yalipo, wanachimba kwa kubahatisha, hata wanapokosa wanahamia kwingineko, wakiacha mashimo na kuharibu miti.

"Uchimbaji mdogo wa madini huwa ni wakubahatisha unakuta mtu amewekeza mtaji wake hata wa shilingi milioni 20, halafu mwisho hawapati madini na mtaji umekatika, unafikiri huyo ataweza tena kufukia mashimo na wakati hana hela? Itabidi atoroke usiku na kuacha mashimo ovyo," anasema Shikome.

Mkurugenzi Msaidizi wa kampuni ya Geita Resources, Yusuph Kulwa, anasema kunakofanyika uchimbaji mdogo, ni lazima kuwapo uharibifu mkubwa wa mazingira, kutokana na matumizi ya zana duni.

Kulwa ambaye ni mtaalamu wa mazingira, anasema wakati mfumuko wa madini ulipotokea katika machimbo hayo, kulikuwapo na watu zaidi ya 20,000 waliokuwa wakifanya uchimbaji holela.

"Wachimbaji wadogo wa madini wanaposikia eneo lina madini huwa wanavamia kila mmoja akitafuta mali, lakini madini yanapokwisha au kupungua eneo hilo huhama na kuacha uharibifu mkubwa wa mazingira, miti ya asili ikiwa imekatwa na mashimo kuachwa bila ya kufukiwa," anasema Kulwa.

"Mwaka jana wakati shughuli za uchimbaji madini zinaendelea ungefika katika eneo hili ungeshuhudia uharibifu mkubwa wa mazingira ambao ulikuwa wepo, kwa kweli tulichakaza hii ardhi ilikuwa hitamaniki tofauti unavyoiona hivi sasa tumepanda miti,"anaongeza Kulwa.

Anafanua kwamba, kutokana na yeye kupata elimu ya kutunza mazingira na baada ya kushuhudia uharibifu mkubwa wa mazingira kutokea na hakuna madini tena, ndipo akashauriana na timu nzima ya uongozi, kwamba ni vyema wakafukia mashimo na kupanda miti ili kutunza mazingira.

Kulwa anaeleza kwamba, kwa sasa ni eneo ambalo wamepanda miti ni hekta 2,000 na wameanzisha vitalu vya miche, ili kila eneo wanakomaliza kufanya shughuli za uchimbaji madini, wapafukie mashimo na kupanda miti.

Valeria Macha kutoka Timu ya Wanasheria watetezi wa Mazingira kwa Vitendo (LEAT), anasema wachimbaji wadogo wakipewa elimu ya utunzaji mazingira na usimamizi wa sheria, wana uwezo mkubwa wa kubadilika, hata kuifanya Tanzania kuwa na uchimbaji madini usio na uharibifu wa mazingira.



# Wamiliki wa shule wabanwa utekelezaji Waraka wa Elimu

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

SERIKALI imesema haitosita kuchukua hatua kwa mmiliki wa shule atakayekaidi au kukataa kutekeleza Waraka wa Elimu Na. 1 wa Mwaka 2023 unaoelekeza kila basi la wanafunzi liwe na wahudumu wa kike na kiume.

Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Omar Kipanga, aliyasema hayo jana bungeni alipojibu maswali ya nyongeza ya Mbunge wa Viti Maalum (CCM), Najma Murtaza Giga.

Mbunge huyo alihoji hatua zitakazochukuliwa kwa wasiotekeleza agizo au maelekezo hayo ya serikali. Pia alisema kutokana na hali ilivyo nchini, kuna haja wasaidizi wa malezi ya watoto majumbani kuwa na elimu ya ulezi wa watoto.

"Je, ni lini serikali itaanzisha chuo cha kuwafundisha vijana wetu ili kupata mafunzo hayo?" Mbunge huyo alihoji.

Akijibu maswali hayo, Kipanga alisema kwa mmiliki wa shule atakayekaidi au kukataa kutekeleza waraka huo, atachukuliwa hatua kwa mujibu wa sheria na taratibu zilizoko. Pia alisema kuwa wizara kupitia VETA imeanzisha kozi mbalimbali ikiwamo za kufundisha wasaidizi wa majumbani wa kike na kiume na serikali itazingatia ushauri wa mbunge wa kuingiza mafunzo ya kulea watoto.

Katika swali la msingi, mbunge huyo alihoji kwanini serikali isiagize kuwe na madereva na kondakta wa jinsia zote kwenye mabasi ya shule ili kudhibiti vitendo vya ubakaji.

Akijibu swali hilo, alisema serikali kupitia waraka huo imetoa maelekezo kwa wamiliki wote wa shule zinazotoa huduma ya usafiri kwa wanafunzi kuhakikisha wanakuwa na mhudumu wa kike na wa kiume katika kila basi au gari linalosafirisha wanafunzi kuanzia mwanzo hadi mwisho wa safari.

"Wizara ilikuatana na wadau wa elimu kujadiliana namna bora ya kutekeleza waraka tajwa na tulikubaliana kwamba tarehe ya mwisho ya kutekelezwa imefutwa.

"Hivyo, wadau wote wanatakiwa kujitahidi kutekeleza waraka huo na kabla ya kupanga tarehe ya mwisho nyingine tutapanga kikao na wadau wote kujadiliana namna ya utekelezaji," alisema.

Hata hivyo, alisema kwa sasa wanahimiza mabasi yote ya wanafunzi yawe na wahudumu wa jinsia zote.

# Serikali yawalipa Bil. 2.4/- wateja 3,446 wa FBME

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

SERIKALI kupitia Bodi ya Bima ya Amana (DIB), imelipa Sh. bilioni 2.43 kama malipo ya awali ya fidia ya bima ya amana kwa wateja 3,446 waliojitokeza wa Benki ya FBME iliyofilisiwa Mei 2017.

Naibu Waziri wa Fedha na Mipango, Hamad Hassan Chande, alibainisha hayo bungeni jana alipojibu swali la Mbunge wa Chwaka (CCM), Makame Mlenge Haji.

Mbunge huyo alitaka kujua tarehe ambayo serikali itawalipa fedha waathirika wa Benki ya FBME iliyofilisiwa miaka sita iliyopita.

Akijibu swali hilo, Chande alisema malipo ya fedha za ufilisi kwa wateja wenye amana zaidi ya Sh. milioni 1.5 yanatokana na uuzaji wa mali, makusanyo ya madeni au mikopo na fedha nyingine za FBME yatafanyika baada ya Mahakama ya Cyprus kutoa uamuzi.

Alisema uamuzi huo unahusu pingamizi lililowekwa na Benki Kuu ya Cyprus la kuitambua DIB kama Mfilisi wa benki yote ikijumuisha makao makuu pamoja na Tawi la Cyprus.

Alisema uamuzi wa mahakama unatarajiwa kutolewa ndani ya mwaka huu wa fedha 2022/2023.



Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Chamwino, Dk. Semistatus Mashimba (kulia), akizungumza wakati akitoa taarifa ya mapato na matumizi ya robo mwaka wa fedha kwenye kikao cha Baraza la Madiwani jana. Wengine ni Mwenyekiti wa Halmashauri hiyo, Edson Swett (wa pili kulia) na Makamu Mwenyekiti, Keneth Yindi. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# DED atoa onyo matumizi fedha za miradi ya elimu

**Na Peter Mkwavila,** CHAMWINO

MKURUGENZI wa Halmashauri ya Wilaya ya Chamwino mkoani Dodoma, Dk. Semistatus Mashimba, ameonya watendaji wa halmashauri hiyo kuhusu matumizi ya fedha za miradi ya elimu.

Akitoa taarifa katika kikao cha Baraza la Madiwani kuhusu fedha zilizotolewa na serikali Sh. bilioni 1.4 kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu ya shule za msingi ndani ya halmashauri hiyo, Dk. Mshimba alisema juzi kuwa zinapaswa kutumika kwa nidhamu ya hali ya juu. "Kamwe fedha hizi hazitochezewa kwa kuwa malengo ni kujenga majengo yenye ubora na imara pamoja na ufanisi mkubwa na ya kisasa," alisema. Aliwaomba madiwani na watendaji kusimamia kwa nidhamu kubwa na kuhakikisha fedha zinatumika kwenye miradi iliyokusudiwa ili kuiunga mkono serikali iliyozitoa kwa ajili ya kuondoa kero ya uhaba wa miundombinu ya elimu. "Hapa ninapenda nisisitize madiwani, watendaji wote ndani ya kata, vijiji hadi vitongoji, fedha hizo ninawataka zikafanye kazi iliyokusudiwa na sivyo vinginevyo. Kila mmoja wetu akasimamie kwa uadilifu katika nafasi yake," aliagiza.

"Serikali yetu chini ya Rais Samia imetuelekeza kwa pamoja na madiwani wa halmashauri kuhakikisha hadi kufikia Juni 30 mwaka huu, miradi hiyo iwe imekamilika kwa asilimia 100 na watoto wasome," aliongeza.

Mkurugenzi huyo alitaja baadhi ya shule ambazo zitakafikiwa kupitia fedha hizo ni pamoja na Shule za Msingi Dabalo, Kwahemu, Malecela Nyamigoha Majengo Mapya na Mazengo, zote za Halmashauri ya Wilaya ya Chamwino.





# Wafanyakazi watelekezwa uwanjani Mei Mosi

**Na Nebart Msokwa,**
MBEYA

ZAIDI ya wanachama 70 wa Chama cha Wafanyakazi wa Serikali za Mitaa (TALGWU) Wilaya ya Mbeya, juzi walitelekezwa na viongozi wao katika Uwanja wa Kumbukumbu ya Sokoine jijini hapo bila kulipwa posho wala kupatiwa chakula.

Wafanyakazi hao ambao ni watendaji wa vijiji na kata, maofisa kilimo na wa idara ya afya, walitelekezwa na viongozi wao baada ya kuhitimishwa kwa maadhimisho ya Siku ya Wafanyakazi Duniani (Mei Mosi). Wafanyakazi hao waligoma kutoka ndani ya uwanja huo mpaka viongozi wa mkoa walipoingilia kati.

Wakizungumza na waandishi wa habari, watumishi hao walisema viongozi wao waliwatoroka na kuwaacha bila kuwapa nauli za kurudia kwenye vituo vyao vya kazi na wakazima simu jambo ambalo liwafanya wabaki hapo.

Mmoja wa watumishi hao, Osia Mwaluwanda, alisema watumishi wenzao kutoka katika wilaya zingine zote za mkoa wa Mbeya walikuwa wamelipwa posho zao na kuondoka isipokuwa wao.

Alisema awali waliahidiwa wangelipwa posho na kupewa chakula cha mchana lakini baada ya maadhimisho kumalizika, mwenyekiti wao aliwatoroka na akazima simu jambo ambalo liliwakera na kuamua kubaki hapo.

Mwaluwanda alisema miaka yote wamekuwa wakiwahujumu kwa kuwapatia posho ya Sh. 2,500 ambazo hazitoshi hata kufika kwenye vituo vyao vya kazi lakini mwaka huu waliwaahidi kwamba wangewalipa lakini haikuwa hivyo.

"Sisi tunachotaka ni tupewe haki yetu. Watumishi wote unaotuona hapa kwa mwaka kila mmoja anakatwa kwenye mshahara wake zaidi ya Sh. 100,000 lakini fedha hizo hatuoni kazi yake. Tunataka hizo posho kwa sababu ni haki yetu," alisema.

Naye Isabela Natales alisema miaka yote wao ndio wanakuwa wa mwisho kutoka kwenye eneo la maadhimisho kutokana na viongozi wao kutengeneza mivutano ambayo inakuwa haina maana yoyote kwao.

Alisema waliambiwa kuwa chakula kingekuwapo lakini walipokwenda kwenye ukumbi walioambiwa walikuta hakuna chakula wala viongozi wao hawapo jambo ambalo liliwakera.

Alisema wao hawaelewi fedha zao ambazo wamekuwa wakikatwa kila mwezi zinapelekwa wapi kama vitu vidogo kama posho na chakula hawapatiwi.

"Sisi hapa hatutoki mpaka tupate haki yetu, wilaya zingine zote wenzetu wamepewa posho zao na wameondoka isipokuwa sisi tu ndio tumebaki tunakuwa kama 'wajinga' tutasubiri hapahapa mpaka waje watupatie haki zetu," alisema.

Miriam Mfinanga alisema walijiunga kwenye chama hicho kwa moyo bila kulazimishwa lakini mwenendo wa viongozi wao unawafanya wajute kujiunga nacho na hata kutamani kifutwe ili wajiunge na vyama vingine.

Alisema mbali na viongozi wao kutoroka pia waliwatolea lugha ya matusi wakati wakijaribu kuwahoji kuhusu baadhi ya mambo ya chama hicho.



Mjumbe wa Halmashauri Kuu ya Chama Cha Mapinduzi (NEC) Taifa, Ndele Mwaselela (katikati), akizungumza na baadhi ya wazee wa Jiji la Mbeya juzi, kuhusu mambo mbalimbali ya maendeleo. Kulia ni Mwenyekiti wa Wazee wa Jiji hilo, Isakwisa Mwam bulukutu na Chifu wa Wasafwa, Rocket Mwansinga. **PICHA: NEBART MSOKWA**

## Vijana wapewa mbinu kujiepusha utegemezi

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

UBUNIFU wa miradi ya kusaidia kujiajiri na kuajiri watu wengine, ni chachu kwa vijana katika kujikwamua kiuchumi, imeelezwa.

Hatua hiyo imeelezwa kuwa itabadili fikra za vijana na kuacha kuendelea kusubiri kuajiriwa na serikali kwa kuwa ajira kwa sasa ni chache kuliko idadi ya wanaozihitaji.

Mjumbe wa Halmashauri Kuu ya Taifa (NEC) ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) anayewakilisha Mkoa wa Mbeya, Ndele Mwaselela, aliyasema hayo juzi alipozungumza na baadhi ya vijana wa chama hicho kuhusu mambo mbalimbali, yakiwamo ya uchumi.

Mwaselela alisema ziko fursa mbalimbali za kiuchumi ambazo vijana wanaweza kuzichangamkia na kuwapatia ajira za kudumu kuliko kuendelea kutembea na bahasha mitaani wakitafuta ajira.

Alisema kwa mkoa wa Mbeya, baadhi ya fursa ambazo vijana wanaweza kuzichangamkia kuwa ni kilimo na ufugaji kwa kuanzisha miradi ya vikundi.

"Mkianzisha miradi ambayo inaeleweka mimi nitakuwa tayari kuwasaidia. Nendeni Mbarali mkakodi mashamba mlime mpunga mimi nitawasaidia pale mtakapokuwa mnakwama. Nawaambia mkijikita huko hamtatamani kuajiriwa," alisema Mwaselela.

Alisema kwa wale ambao wanapata fursa ya kuajiriwa, wanatakiwa waajiriwe na wafanye kazi kwa bidii lakini kwa wale ambao wanaona ajira zinakuwa ngumu ni vizuri wakajiajiri.

Kwa sasa, alisema serikali imeweka mazingira rafiki ya vijana kujiajiri na kuna mikopo ambayo inatolewa, hivyo ni vizuri wakachangamka ili wanufaike na mazingira hayo na wawe miongoni mwa makundi yanayochangia vizuri pato la taifa.

# Serikali yasitisha ujenzi bweni la wasichana

**Na Nebart Msokwa, MBEYA**

SERIKALI imesitisha kutoa fedha za kuendeleza ujenzi wa bweni la wasichana katika Chuo cha Maendeleo ya Jamii Uyole jijini Mbeya, kutokana na utekelezaji wa mradi huo kutofuata ratiba ya matumizi ya fedha zilizotolewa awali.

Katika bajeti ya mwaka wa fedha 2022/23, serikali kupitia Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, imeshatoa zaidi ya Sh. bilioni 1.2 kwa ajili ya ujenzi wa bweni hilo lakini utekelezaji bado unasuasua.

Hayo yalibainika juzi wakati wa ziara ya Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalumu, Amon Mpanju ambaye alitembelea chuo hicho kwa lengo la kuangalia maendeleo ya ujenzi wa miundombinu.

Akitoa taarifa ya mradi huo, Katibu wa Kamati ya Ujenzi wa Bweni hilo, Jackson Msigwa, alisema mradi huo umekuwa ukikabiliwa na matatizo mbalimbali ambayo yamekuwa yakisababisha usikamilike kwa wakati kama ambavyo ilikuwa inakusudiwa.

Alisema wakati wa kiangazi walikuwa wanashindwa kuendelea na ujenzi kutokana na upungufu wa maji kwa maelezo kuwa maji yalikuwa hayatoki kwenye mabomba licha ya kutoa taarifa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mbeya.

Alisema baada ya mvua kuanza kunyesha tatizo la maji lilipungua kutokana na kuanza kutumia maji ya mvua lakini likaibuka tatizo lingine la kiufundi akieleza kuwa wakati wa mvua mradi huo hauwezi kuendelea.

"Wakati wa mvua kubwa huwezi kuendelea kujenga jengo hili. Ghorofa linapojengwa linatakiwa kusiwe na mvua kubwa, kwa hiyo haya ndiyo matatizo ambayo yanatukabili kwenye mradi huu, kiangazi maji hamna na kipindi cha mvua," alisema Msigwa.

Kutokana na matatizo hayo, Mpanju alisema kitendo cha kuchelewa kukamilisha mradi huo katika awamu ya kwanza kinasababisha fedha kwa ajili ya awamu inayofuata kuchelewa pia hali ambayo inakwamisha mradi mzima.

Aliuagiza uongozi wa chuo hicho kupeleka maombi katika Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) kwenda kufanya tathmini ya athari za kimazingira za mradi huo na wapewe cheti ili waendelee kujenga.

Mpanju aliagiza pia kichimbwe kisima ambacho kitakuwa kinatumia wakati wa kiangazi ambapo maji ya bomba yanakuwa adimu ili kutokwama kwa mradi huo huku pia akiwataka kuvuna maji ya mvua na kujaza kwenye shimo lililoko eneo hilo.

"Ni bora tukajaza maji kwenye magari yaletwe hapa kuliko kukwamisha mradi, ni bora hata tukaongeza fedha za mradi lakini kazi ikawa inaonekana, kwa sasa hazitaletwa fedha zingine mpaka zilizoletwa awali zionekane zimefanya kazi gani," alisema Mpanju.

Mkurugenzi wa Ununuzi na Ugavi kutoka wizarani, Martha Chuma, aliwataka wajumbe wote wa kamati ya ujenzi ya bweni hilo kushirikiana kwa njia mbalimbali ili kuhakikisha mradi unakamilika kwa wakati na wanafunzi waanza kulitumia.

Aliwataka pia kuhakikisha wanazingatia ubora wa jengo hilo ambao utaendana na thamani halisi ya fedha ambazo zinatolewa na serikali pamoja na kuwa na uwajibikaji wa pamoja.





# Othman azitaka taasisi za fedha kukabili mabadiliko ya tabianchi

**Na Mwandishi Wetu**

MAKAMU wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar, Othman Masoud Othman, amezitaka taasisi za fedha kujipanga vyema kuisaidia jamii katika kupata shughuli mbadala ili kuachana na ukataji miti kwa upatikanaji wa nishati ya mkaa na kuharibu mazingira.

Othman aliyasema hayo kwa nyakati tofauti alipokutana na kuzungumza na viongozi wa taasisi za fedha na wa Idara Maalum za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar (SMZ), ofisini kwake Migombani kuhusu utekelezaji wa mpango jumuishi wa serikali wa kuirithisha Zanzibar kuwa ya kijani.

Alisema kufanya hivyo kutaisaidia jamii ya Wazanzibari, hasa vijana, kuachana na ukataji miti kwa ajili ya upatikanaji nishati ya mkaa jambo ambalo limekuwa chachu kubwa ya uharibifu wa mazingira nchini.

Makamu wa Rais alisema shughuli ni pamoja na kuwaandalia wananchi fursa na mipago bora ya kazi za uzalishaji ili kujikimu kimaisha na kuwa na fikra mpya za kupenda kupanda na kuitunza miti na hatimaye kuifanya Zanzibar kuendelea kuwa na uoto wa kijani ambao ni wa asili.

Pia alisema kwamba licha ya taasisi hizo kuwa na mipango kadhaa na mizuri kuhusu kuunga mkono suala la kuhifadhi mazingira, pia zina fursa kubwa ya kutengeneza bustani kubwa na kupewa majina ya taasisi zao ili kusaidia kujitangaza na kupata kuungwa mkono zaidi na wananchi.

Alisema utaratibu kama huo umekuwa ukitumika katika nchi mbalimbali duniani ikiwamo Singapore jambo linalosaidia sana taasisi za aina hiyo kujitangaza na kuwa karibu zaidi na jamii.

Kwa mujibu wa Othman, hivi sasa Zanzibar inaendelea kukumbwa na changamoto kubwa ya kimazingira kama zilivyo nchi nyingi duniani kutokana na mabadiliko ya tabianchi jambo ambalo linahitaji juhudi za kila mwananchi na wadau mbalimbali katika kukabiliana nalo.

Wakati huo huo, Othman alikutana na Balozi mpya wa Marekani nchini Tanzania, Michael Battle, aliyefika ofisini kwake na kueleza kwamba mfumo sahihi wa uchaguzi ndio unaoleta uwajibikaji bora kwa viongozi na watendaji mbalimbali katika nchi yoyote duniani.

Naye Balozi Battle alisema nchi yake inaendelea na ushirikiano na Tanzania ikiwamo Zanzibar katika maeneo mbalimbali ya kuleta uwekezaji na biashara za aina mbalimbali hasa kwa kuzingatia Zanzibar hivi sasa inaendeshwa kwa mfumo wa Serikali ya Umoja wa Kitaifa ambao umeleta umoja, mshikamano na utulivu wa kisiasa.



Wadau mbalimbali wa sekta ya habari nchini wakimsikiliza Rais wa Zanzibar Dk. Hussein Ali Mwinyi (hayupo pichani), wakati akihutubia katika maadhimisho ya miaka 30 ya Siku ya Uhuru wa Vyombo vya Habari Duniani, katika Wilaya ya Magharibi "B" Unguja jana. **PICHA: IKULU**

# ZHC yatiliana saini mkataba makazi bora

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

KATIKA kuwapatia makazi bora wananchi, Shirika la Nyumba la Zanzibar (ZHC) limetiliana saini makubaliano ya ujenzi wa nyumba na kampuni ya Simba Development ya Dar-es-Salaam katika eneo la Mombasa kwa Mchina, Zanzibar.

Mkurugenzi Mkuu wa ZHC, Mwanaisha Ali Said, akizungumza jana baada ya utiaji saini wa kuanza kwa mradi huo, alisema mradi huo unatarajiwa kuchukua takriban miezi 15 hadi kumalizika na kwamba nyumba 72 zitajengwa.

Alisema mradi huo unatarajiwa kugharimu Sh. bilioni 9.8 na shirika litatoa Sh. bilioni tatu na fedha zingine zitatolewa kutoka mfuko mkuu wa serikali.

Pia alisema baada ya kumalizika kwa ujenzi, nyumba hizo zitauzwa kwa wananchi watakaozihitaji kwa bei tofauti. Alisema nyumba hizo zitakuwa za vyumba vitatu na zingine vyumba viwili.

"Huu ni mradi wa kwanza wa ujenzi wa nyumba za makazi unaotarajiwa kutekelezwa katika kipindi cha uongozi wa Rais Dk. Hussein Ali Mwinyi. Baadhi ya fedha zimetolewa na shirika na zipo ambazo zimetolewa na serikali kuu," alisema.

Meneja wa Kampuni ya Simba Development, Nurdin Hussein, alisema amefurahishwa na uamuzi wa ZHC kwa kitendo cha kuwaamini hatua ambayo imesababisha kuwapatia kazi ya kutekeleza mradi huo mkubwa.

Aliahidi kutekeleza kazi hiyo kwa kuzingatia uwezo na ubunifu katika usanifu wa majengo ya makazi ya wananchi na kukidhi mahitaji ya makazi bora.

Waziri wa Ardhi na Maendeleo ya Makazi, Rahma Kassim Ali, alisema ujenzi wa nyumba za makazi ni mwendelezo wa ahadi za serikali inayotokana na utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya Chama

Cha Mapinduzi ya mwaka 2020-2025 ya kuwapatia wananchi makazi bora.

Alisema ujenzi wa nyumba za makazi utaendelea kufanyika katika maeneo mbalimbali ya Unguja na Pemba kwa kadri ya hali ya uwezo wa shirika pamoja na serikali.

# Barabara maeneo ya utalii kujengwa lami

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

SERIKALI ya Zanzibar imeamua kujenga barabara zote zinazokwenda katika maeneo ya utalii Nungwi na Kendwa kutokana na sekta hizo kuchangia sehemu kubwa katika uchumi wa Zanzibar.

Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi, Dk. Khalid Salum Mohamed, alisema hayo juzi alipofanya ziara ya kukagua barabara zilizoko katika eneo la Nungwi, mkoa wa Kaskazini Unguja.

Dk. Khalid alisema kilomita 12.5 za barabara zinazotoa huduma katika maeneo ya utalii zitajengwa katika eneo la Nungwi ili kuondoa changamoto inayowakabili wananchi na wawekezaji wa hoteli katika maeneo hayo.

Baada ya kukagua barabara hizo, waziri alisema serikali itaanza kuzijenga barabara zinazoenda katika hoteli ya Zalu na ile inayokwenda katika eneo la Uwanja wa Ndege wa Nungwi kwa hatua ya awali. Alisema serikali itaanza na barabara hizo kutokana na urahisi wake huku ikiendelea kufanya uchunguzi kwa barabara zilizokuwapo katika maeneo ya makazi ya wananchi ili kuona namna bora ya kuyaondosha maji kwa kujenga misingi ya kupitishia maji.

"Tumeamua kuanza na barabara zile mbili ambazo hazina changamoto. Wataalamu wetu wanahitajika kufanya uchunguzi zaidi kwa barabara zinazopita katika makazi ya wananchi kwani pia ziko baadhi ya nyumba italazimika kuondoshwa kabisa ili kufanya utanuzi wa barabara," alisema.

Aidha, Waziri huyo alisema tayari Rais Dk. Hussein Ali Mwinyi ameshatoa maelekezo ya kujengwa barabara zote zinazokwenda katika maeneo ya utalii katika kiwango bora kwa kuziwekea misingi ya kupitishia maji.

Wakati huo huo, Waziri alifika Kibele mkoa wa Kusini Unguja ili kujionea vifaa vitakavyotumiwa na Kampuni ya URKUN kujenga barabara mbalimbali zikiwamo za Jumbi - Tunguu, Charawe- Ukongoroni- Bwejuu na kujiridhisha juu ya uwapo wa lami ya kutosha kwa ajili ya ujenzi wa barabara hizo.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTEA KWA BARUA YA OFA YA KIWANJA

**SELEMAN MAJILU** anatangaza kupotea kwa barua ya ofay a kiwanja **NO. 24 BLOCK A VI** kilichopo kirumba kati. Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

POLISI

**TAARIFA:KIR/RB/4207/2023**

## TANGAZO KUPOTELEWA KADI YA PIKIPIKI

**Shokolo Masanja Gwisu** anatangaza kupotelewa na kadi ya Pikipiki aina ya Lifani yenye namba za usajili T.949 ASY.

Kwa yeyote takaeiona atoe taarifa kituo cha Polisi kilichopo karibu au awasiliane na Shokolo Masanja Gwisu kwa simu namba **0753254746.**

Taarifa ya **Polisi/SHI/SHI/RB/148549/2023.**


## KUPOTEA KWA CHETI



**KENNEDY JOHN** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S0778-0118** kilichotolewa na baraza la mitihani la taifa kupitia **SONGE SECONDARY SCHOOL mwaka 2003.** Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

**POLISI TAARIFA: DAR/STA/RB/121415/2023**

## KUPOTEA KWA VYETI



**JAMES IBRAHIM SHEMDOE** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S0329/0098** kilichotolewa na baraza la mitihani la taifa kupitia **SHULE YA SEKONDARI MAKUMIRA** mwaka 1986 na cheti cha kidato cha sita chenye index namba S0329/0517 kilichotolewa na baraza la mitihani la taifa kupitia **SHULE YA SECONDARI MAKUMIRA** mwaka 1989. Kwa yeyote atakaeviona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

**POLISI TAARIFA: MTW/MTW/RB/142410/2023**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**BONIFACE NDEGE KIRIGIA** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari yenye usajili namba: **T 927 ANW,** CHASSIS NAMBA: **SALLDHMC7HA900038** na ENGINE NAMBA: **16130879A,** Kwa yeyote atakaeviona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

POLISI TAARIFA:

**ARU/ARU/RB/151253/2023**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**THOBIAS CHARLES MASSAWE** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari yenye usajili namba: **T761 CBS.** kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

POLISI TAARIFA:

**ARU/ARU/RB/151574/2023**

## TANGAZO KUPOTELEWA KADI YA GARII

**DANIEL WILHELM LENGAKI** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari aina ya LAND ROVER 110 DEFENDER yenye usajili namba ; T 142 DKT , CHASSIS NAMBA: SALLDHAF71A604314 na ENGINE NAMBA: SALLDHAF71A604314.

Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

**POLISI TAARIFA:**

**KW/RB/1963/2023**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**

**Katika Mahakama ya Mwanzo ya Wilaya DODOMA MJINI**

**Kituo cha CHAMWINO Mkoa DODOMA**

**Usimamizi wa mirathi Na. 23/2023**

**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA MAREHEMU ALLY MOHAMEDI wa Dodoma**

**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOLETWA NA JAWA HUSSEIN HASSAN**

**TANGAZO**

**(Kanuni ya 5(2) ya Kanuni za Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya Marehemu tajwa hapo juu, wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 05 Mwezi 05 Mwaka 2023 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

**Zingatia;**
Endapo kuna yeyote mwenye wosia wa Marehemu anaweza kuuleta Mahakamani kukaguliwa.
Imetolewa leo Tarehe 27 Mwezi 04 Mwaka 2023.

HAKIMU
MAHAKAMA YA MWANZO
CHAMWINO-MJINI

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**

**Katika Mahakama ya Mwanzo ya Wilaya**

**Kituo cha MJINI Mkoa MOROGORO**

**Usimamizi wa mirathi Na. 40/2023**

**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA MAREHEMU STAMILI ABDALLAH wa MZAMBARAUNI**

**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOTOLEWA NA SHABANI HAMADI**

**TANGAZO**


**(Kanuni ya 5(2) ya Kanuni za Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya Marehemu tajwa hapo juu, wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 15 Mwezi 05 Mwaka 2023 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

**Zingatia;**
Endapo kuna yeyote mwenye wosia wa Marehemu anaweza kuuleta Mahakamani kukaguliwa.
Imetolewa leo **Tarehe 02 Mwezi 05 Mwaka 2023.**

HAKIMU
MOROGORO

## KUPOTEA KWA VYETI



**LILY MICHAEL ASECHECK,** anatangaza kupotea kwa cheti cha Kidato cha Sita chenye Index namba **ACSEE.S.0681-0630** kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia **IVUMWE SECONDARY SCHOOL** Mwaka 2019. Kwa yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. Taarifa ya Polisi **MBY/CHU/RB/150200/2023.**

**JAMHURI YA MUUNGANO W A TANZANIA**
**MAHAKAMA KUU YA TANZANIA**
**KANDA YA MOROGORO**
**SHAURI LA MAOMBI MADOGO YA MADAI NA. 22 YA 2022**

**ANTHONY CHIKOTI......................MWOMBAJI**
**DHIDI YA**
**WILLIUM BEATUS LIMBE ................. MJIBU MAOMBI**

**WITO WA MAHAKAMANI**

**KWA: WILLIUM BEATUS LIMBE**
Wito huu ni wa kesi tajwa hapo juu, ambayo imepangwa kutajwa tarehe 29 mwezi wa 5 mwaka 2023 saa 03:00 asubuhi mbele ya Mheshimiwa **Jaji M.J. CHABA.**
Unatakiwa kuhudhuria wewe binafsi au wakili uliyemuidhinisha kusimama kwa niaba yako na pia unatakwia kutoa maelezo yako siku hiyo na nakala zote za ushahidi utakazo tumia kwa shauri hili .
Zingatia kwamba , kutohudhuria siku ya kesi na kwa wakati uliotajwa hapo juu, Mahakama itaendelea kusikiliza shauri hili na kutoa maamuzi bila ya uwepo wako.
Imetolewa chini ya Muhuri wa Mahakama Kuu Kanda ya Morogoro leo siku ya tarehe **2 mwezi wa 05 Mwaka 2023 .**

NAIBU MSAJILI MAHAKAMA KUU
MOROGORO

**THE LAND REGISTERATION ACT(CAP.334)LOSS OF CERTIFICATE OF TITLEF:34395REGISTERED OWNER: PAUL NDEMBWELE NDIMBO OF P.O.BOX316,SONGEALAND: PLOT NO 437BLOCK "Y:MFANYAKI IN SONGEA TOWNSHIP.APPLICANT:REGINA MATHIAS CHINGUKU (AS Administratix of estate of the late of PAUL NDEMBWELE NDIMBO OF P.BOX316,SONGEATAKE**

NOTICE that the certificate of Title to the land described above is saidto be lost and that lintend to issue new certificate of Title in lieu there of unless cuause to the contrary is shown within one month from the date this Notice is published in the official Gazette.THE ORIGINAL CERTIFICATE OF TITLE if found,should be delivered at the land Registry, P.Box 707,RUVUMA................................ CRISTINA NYEREREASSISTANT REGISTRAR OF TITTLES17 APRIL,2023

17 April, 2023
CHRISTINA NYERERE
ASSISTANT REGISTRAR OF TITLES

**THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**
**MINISTRY OF HOME AFFAIRS**
**IMMIGRATION DEPARTMENT**
**APPLICATION FOR TANZANIA CITIZENSHIP**



**Notice is hereby given that,**
**Mr. JOHN RICHARD FURTER**

Whose photograph provided above is applying to the Minister of Home Affairs for Tanzania citizenship. His nationality at present is SWITZERLAND. Country of Origin SWITZERLAND. His occupation is BOARD CHAIRMAN. His employer/Business/Address is P.O. Box 91, ARUSHA. He has been in this country since 2010 apart from ARUSHA Region. He has also resided in ...............Region.
That any person who knows any reasons why citizenship should not be granted to the applicant, should sent a written and signed statement of facts to the Commissioner General of Immigration Services. P.O. Box 512, Dar es salaam. Using Ref. No.

FOR:COMMISSIONER GENERAL OF IMMIGRATION SERVICES

**KATIKA MAHAKAMA KUU YA TANZANIA**
**MOSHI**
**UTHIBITISHO NA USIMAMIAJI WA MIRATHI**
**SHAURI NAMBARI 04 LA MWAKA 2023**
**MAOMBI YA BARUA ZA USIMAMIAJI WA MIRATHI YA:**
**JOHN BOSCO SEMALI...............MAREHEMU**
**NA**
**MRS. EFGENIA BOSCO SEMLI NA LUCAS BOSCO SEMALI..................WAOMBAJI**
**TAARIFA YA KAWAIDA**
**(Kanuni ya 75)**

Watu wote wanaodai kuwa na haki katika Mirathi ya marehemu aliyetajwa hapo juu wanafahamishwa kufika na kuangalia mashauri haya katika jalada kama wanaona inafaa kabla ya kutolewa kwa barua za usimamiaji wa Mirathi kwa muombaji aliyeomba hapo juu.
Mapingamizi yoyote kuhusu maombi haya yote yameandikishwa mnamo au kabla ya tarehe 12 mwezi wa sita, mwaka 2023.
Imewasilishwa Moshi leo tarehe 5 Mwezi wa Nne, Mwaka 2023.

NAIBU MSAJILI
MAHAKAMA KUU MOSHI
HIGH COURT OF TANZANIA
MOSHI

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**Katika Mahakama ya Mwanzo ya Wilaya Morogoro**
**Kituo cha Mjini Mkoa Morogoro**
**Usimamizi wa mirathi Na. 41/2023**
**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA MAREHEMU OMARY ALLY MAULID WA MJI MPYA**
**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOTOLEWA NA ALLY OMARY NYAWENGA**
**TANGAZO**
**Kanuni ya 5 (2) ya kanuni za Usimamizi w a Mirathi Mahakama za Mwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote /maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu , wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe **23 mwezi 5 Mwaka 2023** kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa Msimamizi wa Mirathi hiyo.
**Zingatia;**
Endapo kuna yeyote mwenye Wosia na Marehemu anaweza kuuleta Mahakamani kukaguliwa.
Wosia wa marehemu huyo upo Mahakamani na waweza kukaguliwa .
Marehemu hakuacha wosia * Futa isiyohusika
**Imetolewa tarehe 2 mwezi 05 mwaka 2023**

HAKIMU
MAHAKAMA YA MWANZO
MOROGORO

IN THE DISTRICT COURT OF DODOMA
AT DODOMA
Probate & Administration Cause No...OF 2023
In the matter of the Estate of the late
**TANASIO CHARLES USELE**
And
In the matter of an application for letters of administration by **ROBERT TANASIO USELE.**

**GENERAL CITATION**
**(Made under Rule 75 of Probate Rules, Cap 352 R.E 2002)**

**All PERSONS** claiming to have any interest in the Estate of the above- named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above- named Petitioners.
Objections to the grant should be filed on or before the 31 Day of 05, 2023
Dated at Dodoma this 28 day of 4, 2023

RESIDENT MAGISTRATE

RE: THE LAND ACT NO 4 OF 1999

**LOSS OF ORIGINAL LETTER OF OFFER**

**LOSS OF ORIGINAL LETTER OF OFFER OF;**
**RE: NO. AR/MAN/144/JJ, of 14 JUNE 2007**
**REGISTERED OWNER: SALUMU ABDALLAH MKUYA**

**LAND: PLOT N. 144 BLOCK "JJ" LOCATION MIEMBENI MANYONI DISTRICT**
**APPLICANT: SALUMU ABDALLAH MKUYA**

**TAKE NOTICE** that the **ORIGINAL LETTER OF OFFER** to the land described above is said to be lost and that I intend to issue a **REPLACEMENT OF THE ORIGINAL OF OFFER** in lieu thereof unless cause to the contrary is shown thirty days from the date of this publication.

The **ORIGINAL LETTER OF OFFER** is found, should be delivered to the office of the District Director, Manyoni District Council P.O. Box 60, Manyoni.
Issured by

Mariam Simoni Mavunde
For: - DISTRICT DIRECTOR
MANYONI
DISTRICT LAND OFFICER
MANYONI

**Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa Tupigie 0677020701**

**TAHADHARI:** Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji **THE GUARDIAN LIMITED** hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

HABARI KIMATAIFA

VITA RUSSIA, UKRAINE

# Sasa zajiweka sawa kwa mapambano

**KYIV,** Ukraine

SERIKALI ya Ukraine imetangaza hali ya tahadhari katika mji wa Kherson, ulioko karibu na eneo la mapambano kusini mwa nchi hiyo.

Tangazo hilo limetolewa na mkuu wa utawala wa kijeshi wa Kherson, Oleksandr Prokudin, wakati vikosi vyake vikijiandaa na mashambulizi ya kupambana na wanajeshi wa Russia katika majira ya machipuko.

Katika mtandao wa Telegram, Produkin alisema kuanzia muda wa jioni ni marufuku watu kutembea kwenye mji huo.

Aidha, raia watatu wameuawa katika shambulizi lililofanywa na Russia lililotokea jana kwenye soko kubwa katika mji wa Kherson.

Wakati huo huo, Idara ya Usalama ya Shirikisho la Russia, FSB, lilisema kuwa watu saba wanaohusishwa na shirika la kijasusi la Ukraine wamekamatwa katika jimbo la Crimea.

**Wakati huo huo, Idara ya Usalama ya Shirikisho la Russia, FSB, lilisema kuwa watu saba wanaohusishwa na shirika la kijasusi la Ukraine wamekamatwa katika jimbo la Crimea.**

FSB ilisema mashambulizi dhidi ya Sergei Aksyonov, gavana wa jimbo hilo linaloungwa mkono na Russia, pamoja na maofisa wengine, yamezimwa.

Katika hatua nyingine, Russia imetangaza kuwa itapunguza sherehe za mwaka huu za siku ya ushindi.

Maofisa wa nchi hiyo walielezea sababu za kupunguza sherehe hizo ni kutokana na matisho ya mashambulio kutoka kwa vikosi vinavyounga mkono Ukraine.

Milipuko na moto ilitokea nchini humo katika wiki za hivi karibuni, lakini baadhi walidai kuwa kupunguzwa kwa matukio hayo inaonyesha kuwa nchi hiyo inahofia sherehe hizo zitabadilika na kuwa majukwaa ya maoni tofauti dhidi ya uvamizi wa Ukraine.

Sherehe hizo ambazo hutawaliwa na maonyesho ya kuvutia ya kijeshi kwa kawaida huadhimisha Siku ya Ushindi, ambayo ni kumbukumbu ya ushindi wa Muungano wa Usovieti dhidi ya Wanazi wa Ujerumani Mei 9, 1945.

Moja ya onyesho linalotambulika zaidi ni lile la maandamano ya kikosi kisichoweza kufa, ambapo watu nchini humo huandamana huku wakiwa wameshika picha za ndugu na jamaa zao waliopigana vita kuu ya pili ya dunia.

Mwaka jana, Rais Vladimir Putin aliongoza maandamano katika eneo la Red Square mjini Moscow huku akiwa ameshikilia picha ya baba yake akiwa amevaa magwanda ya jeshi.

Wakati huo huo, Muungano wa Ulaya unaazimia kutenga zaidi ya euro milioni 500 kwa ajili ya kuongeza uzalishaji wa makombora na mizinga ili kuisaidia Ukraine na kujaza hifadhi yake.

Mpango wa kamati ya Muungano wa Ulaya, ambao utatangazwa Jumatano ijayo, unatoa ruzuku kwa makampuni ya silaha ya Ulaya, ambayo yataweza kuwekeza katika sekta ya makombora aina ya howitzer na ndege roketi, uzalishaji silaha za kemikali na kuzibadilisha silaha za zamani kuwa za kisasa.

"Inapokuja katika suala la ulinzi, sekta yetu lazima ibadilike na kuwa ya utawala wa uchumi wa vita," alisema Kamishna wa Ulaya anayehusika na soko la ndani, Thierry Breton.

Iwapo mpango huo mpya utaidhinishwa na nchi zote wanachama wa Ulaya na Bunge la Ulaya, utakuwa ni sehemu ya juhudi kubwa za kuipatia Ukraine silaha.

Kamishna wa Muungano wa Ulaya alikiri kuwa, licha ya uwepo wa ukubwa wa sekta ya viwanda vya silaha barani humo, nchi wanachama hazina kiwango cha silaha kinachoweza kukidhi mahitaji ya usalama wa Ukraine na nchi husika. **DW**



Wafanyakazi wa meli ya mafuta yenye bendera ya Gabon wakiokolewa na wahudumu wa ukoaji wa Malaysia baada ya meli hiyo kushika moto kwenye pwani ya kusini ya nchi hiyo juzi. Wafanyakazi 25 waliokolewa kutoka ndani ya meli hiyo na shughuli za utafutaji zinaendelea kwa watu watatu waliopotea. Meli hiyo ilikuwa ikielekea Singapore kutoka China. **PICHA: EPA-EFE**

## Maporomoko ya ardhi yaua 100 Rwanda

**KIGALI,** Rwanda

ZAIDI ya watu 100 wamefariki nchini Rwanda, baada ya mvua kubwa kunyesha usiku wa kuamkia juzi katika maeneo ya magharibi mwa nchi hiyo.

Shirika la utabiri wa hali ya hewa la Rwanda limeonya juu ya kuwapo kwa mvua kubwa mwezi Mei. Gavana François Habitekego alisema takwimu walizonazo ni kwamba watu 55 walikufa kwa kuangukiwa na nyumba zao.

Habitekego alisema kuwa watu wengi walifariki katika wilaya ya Ngororero, lakini "wapo waliopoteza maisha katika maeneo ya Rubavu, Rutsiro na Karongi.

Jimbo la Magharibi na kaskazini mwa Rwanda ni maeneo yenye milima ambayo mara nyingi huathiriwa na maporomoko ya ardhi wakati wa misimu ya mvua.

Mamlaka ya Hali ya Hewa ya Rwanda hivi majuzi ilionya kuwa kutakuwa na mvua kubwa mwezi huu.

Wizara ya Maafa iliwatahadharisha wananchi kuwa waangalifu wakati mvua zinanyesha katika maeneo tofauti nchini humo.

Gavana Habitekego aliiambia BBC kwamba barabara nyingi zimeharibika kwa kukatika na kufunikwa na matope hivyo ni vigumu kutembea. Barabara kuu katika jimbo la magharibi ya Kivu Belt inayounganisha miji ya Rubavu – Karongi, Muhanga hadi Musanze na barabara ya Musanze kwenda Rubavu zimeharibika.

"Sehemu nyingine zimefunikwa na matope, siwezi kusema kuwa barabara zote hizo zinaweza kutumika," alisema. **BBC**

## Nigeria kuchunguza tambi hatari

**ABUJA,** Nigeria

SHIRIKA la udhibiti wa viwango nchini Nigeria (Nafdac) limesema linachukua hatua ya haraka kuchunguza chakula aina ya tambi kwa madai ya kuwa na kiambata hatari.

Tambi hiyo yenye chapa maarufu ya noodles inadaiwa kuwa na kiungo kinachohusiana na kuongezeka kwa hatari ya mtu kupata saratani.

Shirika hilo lilisema kwenye taarifa yake kwamba linafanya uchunguzi wa sampuli na tathmini ya tambi za Indomie, ikiwa ni pamoja na viungo, ili kuangalia uwepo wa kiambatana aina ya ethylene oxide.

Nafdac ilieleza kuwa uchunguzi huo unafuatia kuondolewa kwa tambi maalum zenye ladha ya kuku wiki iliyopita kwenye masoko ya Malaysia na Taiwan baada ya kiungo cha ethylene oxide kugundulika katika baadhi ya sampuli.

Indofoods, ambayo ni kampuni kubwa ya chakula ya Indonesian inayotengeneza tambi za Indomie, hata hivyo imetetea usalama wa bidhaa zake.

HABARI MICHEZO

# NAMPEPECHE AMTISHIA CHEKA KUMPIGA KWA KO YA MAPEMA

Na Saada Akida

BONDIA wa Ngumi za Kulipwa nchini, Issa Nampepeche, amesema amejiandaa vizuri na kumwonya mpinzani wake, Cosmas Cheka, kwa kumwambia atampiga kwa KO na kumtaka asimkimbie kama ilivyokuwa mwaka 2021.

**Nampepeche ametoa onyo hilo kuelekea katika pambano lao linalotarajiwa kupigwa Mei 27, mwaka huu, jijini Dar es Salaam , ambapo bondia Ibrahim Class, atacheza pambano kuu dhidi ya Said Chino.**

Akizungumza na Nipashe jana, Nampepeche, alisema amejipanga vizuri kuhakikisha anapata ushindi kwenye pambano hilo huku akimpa onyo Cheka kwa kumwambia kuwa ikitokea amekimbia basi italazimika wamkimbize ili kuweza kumaliza utata wao.

Alisema anahofu Cheka anaweza kukimbia tena kwenye pambano lao la Mei 27, mwaka huu, kama alivyofanya mwaka 2021 na kwamba akifanya hivyo ajue watamkimbiza kwa kuwa pambano hili amelitaka mwenyewe.

Nampepeche (pichani) alisema amejipanga vizuri kwa ajili ya kushinda kwa sababu safari hii, mpinzani wake amelitaka mwenyewe pambano na anachokitaka ni kumpa onyo kwa kuwa amefanya maandalizi kwa muda mrefu.

"Safari hii yeye ndiye amelitaka hili pambano, ninachotaka kumwambia ni kwamba akiingia kwenye mitego yangu napiga KO ya mapema ingawa siwezi kusema kwamba itakuwa raundi ya ngapi.

"Mwaka 2021, alikimbia kwa kuja ulingoni na 'hogo' kwa kujifanya amevunjika mkono ila safari hii akijaribu tena kuleta mambo yake ya kukimbia siku ya pambano, tutahakikisha tunamkimbiza ili apande ulingoni tuweze kumaliza huu ubishi," alisema Nampepeche.

Aliongeza Cheka ni bondia hapaswi kuogopa mapambano ambayo mwenyewe ndiye ameyataka hivyo anaamini amejiandaa vizuri, lakini atampiga kwa KO ya mapema tu siku hiyo.



MNAHESABU?...



Kiungo wa Arsenal, Martin Ødegaard, akishangilia moja kati ya mabao yake mawili aliyofunga wakati wakishinda 3-1 dhidi ya Chelsea kwenye mechi ya Ligi Kuu England iliyopigwa Uwanja wa Emirates juzi usiku. **PICHA: MTANDAO**

## Mapinduzi, Kiluvya zakwea Daraja la Pili

Na Adam Fungamwango

TIMU za Mapinduzi FC ya Mwanza na Kiluvya FC ya Dar es Salaam, zimefanikiwa kupanda daraja na kutinga 'First League' (Ligi Daraja la Pili), baada ya kupata ushindi katika mechi zao za nusu fainali ya Ligi ya Mabingwa Mikoa iliyochezwa mwanzoni mwa wiki hii katika Uwanja wa Majengo, Moshi mkoani Kilimanjaro.

Pia, timu hizo zimetinga hatua ya fainali ya ligi hiyo ambapo sasa zinatarajiwa kupambana kusaka bingwa wake.

Katika mechi ya kwanza, Mapinduzi FC, ilifanikiwa kuiondosha Tanesco FC ya Kilimanjaro kwa mikwaju ya penalti 4-1, baada ya timu hizo kumaliza dakika 120 kwa sare ya bao 1-1.

Kocha Mkuu wa Tanesco FC, Dadi Gilbart, alisema walicheza vema, lakini bahati yao wana nafasi nyingine ya kwenda kucheza mechi ya mshindi wa tatu na kama wakishinda, watakwenda kucheza mechi ya mchujo ili kujaribu tena kupanda.

"Tulitaka kuumaliza mchezo kwa dakika 45 za kwanza, lakini hali ilikuwa ngumu, pamoja na kwamba tuliongoza, lakini kipindi cha pili wenzetu wakaja na mpango mkakati wa kutuzuia. Pia nadhani kutokana na mechi mfululizo baadhi ya wachezaji wangu tegemeo walichoka na kukaribisha mashambulizi mpaka wenzetu wakasawazisha," alisema kocha huyo.

Mechi ya nusu fainali ya pili ilikuwa ni kati ya Nyumbu FC ya Pwani na Kiluvya FC, ambapo Kiluvya ya Dar es Salaam ilifanikiwa kutinga fainali na kupanda daraja nayo pia kwa mikwaju ya penalti 7-6, baada ya dakika 120 za suluhu.

Kocha Mkuu wa Kiluvya, Athumani Shija, alisema kama alivyotarajia mechi ingekuwa ngumu ni kweli ilitokea na kwamba ni kutokana na timu zote kuwa za jeshi hivyo wanajuana uchezaji wao, na kama alivyotabiri kuwa ingeamuliwa na makosa madogo madogo au mikwaju ya penalti ndiyo ilivyotokea.

"Tumepambana muda mrefu kupanda daraja, lakini tulikuwa tunafeli, nilisema mechi itakuwa ni ngumu kwa sababu timu zote ni za jeshi na wachezaji wengi wa Nyumbu walikuwa kwetu na mimi ndiyo nilikuwa mwalimu wao," alisema kocha huyo.

# Stand, Cosmopolitan zapanda Championship

Na Adam Fungamwango

TIMU za Stand United na Cosmopolitan zimefanikiwa kupanda daraja na kuingia Ligi ya Championship, huku pia zikitinga fainali ya First League [Ligi Daraja la Pili], baada ya kupata ushindi kwenye mechi zao za nusu fainali zilizopigwa Uwanja wa Azam Complex, Chamazi, Dar es Salaam mwanzoni mwa wiki hii.

Stand United iliyoshuka daraja Ligi Kuu Tanzania Bara msimu wa 2018/19, ilipata ushindi wa mabao 2-1 dhidi ya TMA FC, mechi iliyopigwa kwa dakika 120.

TMA ndiyo ilianza kutangulia kupata bao, lililowekwa ndani ya wavu na David Rweyendela kwa kichwa dakika ya 61, huku Stand United ikisubiri hadi dakika sita kabla ya mechi kumalizika kusawazisha bao lililowekwa ndani ya kamba na Kimu Juma kwa shuti kali na kuifanya mechi hiyo kumalizika kwa sare ya bao 1- 1 kwa dakika 90, kabla ya dakika 30 za nyongeza.

Wakati kila mtu akidhani mechi ingeenda hatua ya matuta, Maulidi Fadhili, aliifungia bao Stand kwa kichwa na kuifanya si tu kutinga fainali ya First League hatua ya nane bora, lakini pia kupanda daraja na sasa itacheza Ligi ya Championship msimu ujao.

Nusu fainali ya pili ilishuhudia Mabingwa wa Tanzania Bara mwaka 1967, Cosmopolitan ikifanikiwa kutinga fainali ya ligi hiyo na kupanda daraja ilipoifunga Dar City mabao 2-1, matokeo hayo yakipatikana ndani ya dakika 90.

Timu zote mbili zilizoingia fainali na kupanda daraja zimetoka Kundi A, ambalo liliongozwa na Stand United na Cosmo kumaliza nafasi ya pili.

ZISIKUPITE

### MESSI KUONDOKA PSG

MSHAMBULIAJI wa Argentina, Lionel Messi, 35, ataondoka Paris St-Germain mwishoni mwa msimu huu baada ya mabingwa hao wa Ufaransa kuamua kutoongeza mkataba wake. ***(FootMercato)***

### UNITED YATAKA WATATU

KLABU ya Manchester United imeainisha nyota wa tatu mbadala wa mshambuliaji wa Tottenham Hotspur na England, Harry Kane, 29, ambao ni mchezaji wa Kimataifa wa Ufaransa na Eintracht Frankfurt, Randal Kolo Muani (24), mshambuliaji wa AS Roma na England, Tammy Abraham miaka 25, na mchezaji wa Kimataifa wa Argentina anayechezea Inter Milan, Lautaro Martinez, 25. ***(FourFourTwo)***

### AKWAMA TOTTENHAM SPURS

MAZUNGUMZO ya Tottenham na kocha wa zamani wa Bayern Munich, Julian Nagelsmann, kuhusu kuwa kocha wao mpya yamekwama kwa sababu ya sintofahamu kuhusu nafasi ya mkurugenzi wa michezo wa klabu hiyo. ***(Telegraph)***

### SAM NA LEEDS WATETA

SAM Allardyce yuko kwenye mazungumzo ya kuwa kocha ajaye wa Leeds United na amepewa bonasi ya pauni milioni moja ikiwa ataibakisha klabu hiyo ya Elland Road kwenye Ligi Kuu England. ***(Star)***

### POCHETTINO KUULA CHELSEA

WAMILIKI wa Chelsea, Todd Boehly na Behdad Eghbali walikutana Los Angeles nchini Marekani mwishoni mwa wiki iliyopita kujadili uteuzi wa kocha wa zamani wa Tottenham Hotspur, Mauricio Pochettino, ili awe kocha ajaye wa klabu hiyo ya Stamford Bridge. ***(Evening Standard)***

### ARTETA KUPEWA KITITA

MMILIKI wa Arsenal, Stan Kroenke, anatarajiwa kumpa kocha Mikel Arteta kitita cha pauni milioni 200 ili kuimarisha kikosi chake msimu wa majira ya joto. ***(Football transfers)***

### RICE KUSEPA WEST HAM

KLABU ya West Ham imeanza kutafuta kiungo mbadala wakijiandaa kumkosa mchezaji wa Kimataifa wa England, Declan Rice, 24, anayesakwa na Arsenal. ***(Football Insider)***

### GUEHI AWANIWA SPURS

KLABU ya Tottenham Hotspur inatarajiwa kupigana vikumbo na mahasimu wao wa London Kaskazini, Arsenal katika mbio za kujaribu kumsajili beki wa Crystal Palace na England, Marc Guehi, 22. ***(Evening Standard)***


### BAYERN KUMUUZA MANE

KLABU ya Bayern Munich iko tayari kusikiliza ofa kwa ajili ya mshambuliaji wa Senegal, Sadio Mane, 31, ambaye alijiunga nao akitokea Liverpool msimu uliopita wa majira ya joto. ***(90Min)***

### JAMES MKATABA MPYA

KLABU ya Fulham inapanga kufanya mazungumzo na Leeds United kuhusu kumpa mkataba wa kudumu winga, Dan James, 25. ***(Football Insider)***

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA



# ARTETA BADO ANAIMANI NA ARSENAL KUTWAA UBINGWA

**LONDON,** England

**Ni mechi nne zimesalia, tuko kileleni kwa sasa tunasubiri kuona kitakachotokea...**

MIKEL Arteta ameitazama timu yake ya Arsenal ikirejea kileleni mwa msimamo wa Ligi Kuu kwa ushindi dhidi ya Chelsea kabla ya kusisitiza kuwa hataruhusu vichwa vya wachezaji wake kushuka.

**'Washikabunduki' hao walikuwa mbele kwa pointi nane mwezi uliopita, lakini walikuwa nyuma ya Manchester City kutokana na mfululizo wa mechi nne bila kushinda ambao ulimalizika kwa ushindi mnono wa mabao 3-1 dhidi ya 'Blues' hao juzi, Jumanne.**

Nahodha Martin Odegaard alifunga mabao mawili na Gabriel Jesus alimalizia ushindi huo kabla ya kipindi cha mapumziko huku bao la kwanza la Noni Madueke la ligi likiwa faraja tu kwa vijana wa Frank Lampard.

Arteta alikataa kuwaondoa Arsenal kwenye mbio za ubingwa na ushindi huu uliwafanya kuwa na pointi mbili - ingawa wamecheza michezo miwili zaidi ya City.

Mhispania huyo alikiri kuwa hataki kuona morali ikishuka baada ya kupoteza kwa Man City na kusababisha uongozi wao kuporomoka.

"Ni mechi nne zimesalia, tuko kileleni kwa sasa," alisema.

"Hatuwezi kufanya hivyo, kuwa hapa tulipo baada ya miezi 10 dhidi ya timu tunayopigana nayo, kuwa pale na kuwa na uwezekano wa kuwa juu - lazima tufurahie na kuikumbatia, kuongeza nafasi ambayo tunayo kwa sababu hatujui kitakachotokea.

"Tulitaka kuwa na mtazamo tofauti sana wa mchezo, na tulifanya hivyo tangu mwanzo.

"Timu imerejea katika ubora wake. Tulitaka kuthibitisha kuwa tuna moto huo. Niliweza kuona hilo katika siku chache zilizopita, na tulijiandaa (kwa) mchezo vizuri.

"Kiakili tulifika katika hali nzuri na kiwango sahihi cha nishati. Kila kitu kilikwenda kwa ajili yetu pia, ambayo ni muhimu.

"Tumekuwa na wiki kadhaa ngumu na michezo tofauti sana, na hisia nyingi zinazohusika. Tumerejea kileleni mwa ligi - tuone kitakachotokea."

SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!
SUPA JACKPOT KWA 1000/- 1,109,9

MECHI KALI
SINGIDA BS FC
VERSUS
YOUNG AFRICANS
1 | 3.69
X | 2.81
2 | 1.80

KUWEKA PESA:
- PIGA *150*87#, CHAGUA 4
- WEKA PESA.
tigo pesa vodacom m-pesa halopesa airtel money
SEND

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
PIGA *150*87#
GBT:0249 18+ HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, PIGA: 0764115588, 0677115588 0685115588
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# RONALDO KURUDI REAL MADRID



**RIYADH,** Saudi Arabia

CRISTIANO Ronaldo anatarajiwa kurejea Real Madrid, miezi mitatu tu baada ya kusajiliwa na Al Nassr.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 38, alikuwa mchezaji anayelipwa mshahara mkubwa zaidi duniani kwa mwezi, baada ya kukubaliana kulipwa pauni milioni 175 kwa mwaka hadi 2025.

Ronaldo alijiunga na miamba hao wa Saudi Arabia, baada ya mkataba wake na Manchester United kuvunjwa, kutokana na mahojiano yake na Piers Morgan.


Lakini ripoti kutoka Hispania zinadai Ronaldo tayari anafikiria kuachana na ligi hiyo ya Saudi Pro.

Kwa mujibu wa El Nacional, 'Los Blancos' hao wako tayari kumpa gwiji wa klabu yao nafasi ya ubalozi, huku mpenzi wake, Georgina Rodriguez, akitamani kurejea Madrid.

Florentino Perez amehakikisha kwamba Ronaldo hatakosa kazi Santiago Bernabeu.

Ronaldo alifunga mabao 451 katika mechi 438 wakati akiwa Real Madrid. Pia alitwaa tuzo mbalimbali akiwa na Los Blancos, ambazo ni pamoja na mataji manne ya Ligi ya Mabingwa Ulaya, makombe matatu ya Klabu Bingwa Dunia, na mataji mawili ya LaLiga.

Tangu atue Al Nassr, Ronaldo ana mabao 12 kwa jina lake, hivi karibuni akifunga katika ushindi wa 3-0 wa timu yake dhidi ya Al Raed, Ijumaa iliyopita.



## Messi asimamishwa PSG

**PARIS,** Ufaransa

LIONEL Messi amesimamishwa na Paris St Germain kwa wiki mbili baada ya kufanya safari isiyoidhinishwa ya kwenda Saudi Arabia, kwa mujibu wa ripoti.

Inasemekana Messi alisafiri baada ya PSG kufungwa nyumbani na Lorient Jumapili bila ruhusa ya klabu.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 35, ambaye ana jukumu la kuwa balozi wa utalii nchini Saudi Arabia, anatarajiwa kukosa mechi dhidi ya Troyes Jumapili na AC Ajaccio, Mei 13, mwaka huu.

Inasemekana hatafanya mazoezi na klabu, au kulipwa, kwa muda wa wiki mbili.

Messi alicheza dakika zote 90 za kipigo cha mabao 3-1 kutoka kwa Lorient na kuwaacha PSG kwa pointi tano tu mbele ya Marseille kileleni mwa Ligue 1.

Nahodha huyo wa Argentina ameifungia klabu yake mabao 24 msimu huu.

75,029/-

# MANDONGA, MMALAWI KUZICHAPA DODOMA

Na Saada Akida

BONDIA wa Ngumi za Kulipwa nchini, Karim Mandonga, anatarajia kupanda ulingoni Juni 24, mwaka huu, dhidi ya Alick Mwenda wa Malawi katika pambano litakalofanyika viwanja vya Chinangali jijini Dodoma.

Mandonga anapanda ulingoni kwenye pambano hilo ikiwa ni miezi miwili tangu amchape Kenneth Lukyamuzi wa Uganda nchini Kenya katika pambano la kuwania mkanda wa Ubingwa wa PST Afrika Mashariki na Kati.

**Akizungumza na Nipashe jana, Mandonga, alisema anatarajia kurejea ulingoni kuzichapa dhidi ya Mwenda wa Malawi katika pambano la raundi nane.**

Alisema anaendelea kufanya mazoezi ya kujiandaa na pambano hilo kuhakikisha anafanya vizuri na kumpiga mpinzani wake kwa raundi ya mapema ikiwezekana kwa KO.

"Nashukuru Mungu nipo sawa natarajia kurejea ulingoni pale Dodoma, hii kwangu itakuwa ni mara ya kwanza kupigana ndani ya Jiji la Dodoma, 'Mandonga Mtu Kazi', niwaambie mashabiki wangu nakuja huko kufanya maajabu.

"Huyo Mwenda anatakiwa ajiandae kweli kwa sababu tayari nimeshaingia kambini kwa ajili ya pambano hilo, anatakiwa kujua nishapiga watu nje na kuipa sifa kubwa Tanzania, basi na yeye nitampiga na kuendelea kuipa sifa nchini yangu katika pambano langu hilo," alisema Mandonga.

Mandonga amekuwa kivutio kikubwa katika ulingo wa masumbwi huku akiwavutia watu wengi katika Ukanda wa Afrika Mashariki kuupenda mchezo huo.

Hiyo ni kutokana na mikwara ambayo amekuwa akiitoa kabla ya kupanda ulingoni jambo ambalo mashabiki wa ngumi wamekuwa upande wake awe ameshinda ama kushindwa na mara nyingi wamekuwa wakieleza wanafurahi zaidi akipigwa maana ndiyo huongeza vibweka vyake.



Mandonga

## Simba yapania kuionesha Azam soka la Morocco

INATOKA UK. 24

halisi na wala hawakubahatisha, na kama watacheza kwa asimilia 80 tu, basi dhahama kubwa itawakumba Azam FC.

"Nikisema hivyo nina maana ni lazima tulinde kiwango chetu, hivi sasa tupo kwenye kilele cha ubora kwa hiyo kila mechi ni lazima tucheze kwa kiwango kile kile, si leo umecheza asilimia 80, kesho 20, kesho kutwa 60, yaani inakuwa ni kama unabahatisha maisha hivi.

"Tunatakiwa tucheze huku kila Mwanasimba akiwa 'anainjoi'. Tunataka kuona mashabiki wetu wakiangalia mechi za timu yetu wawe kama wanaangalia tamthilia tamu ya mahaba, siyo unatazama mpira umeshikilia roho," alisema meneja habari huyo.

Awali, Simba na Azam zilikuwa zicheze mechi hiyo Jumamosi, lakini TFF iliusogeza mbele mchezo huo, huku pia ikiuahirisha mwingine wa nusu fainali kati ya Yanga na Singida Big Stars uliokuwa uchezwe Mei 7, kwenye Uwanja wa Liti, Singida, hadi utakapopangiwa tarehe nyingine, baada ya kulikubali ombi la Yanga ambayo iliiomba mechi hiyo isogezwe mbele ili kupata nafasi ya kujiandaa na mechi ya nusu fainali ya Kombe la Shirikisho barani Afrika dhidi ya Marumo Gallants utakaochezwa Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam, Mei 10, mwaka huu.

## Nabi awaonya Yanga

INATOKA UKURASA 24

fainali, nimewaona na ninaimani vijana wangu watafuata maelekezo niliyowapa na kupata matokeo katika mchezo huo," alisema Pluijm.



Alisema licha ya kupoteza mchezo wa kwanza, sio sababu ya kukubali kupoteza kwa mara ya pili, na kwamba wamejiandaa vizuri kuhakikisha wanautumia vema uwanja wa nyumbani.

Timu hizo zinakutana kwa mara ya pili msimu huu wa Ligi Kuu baada ya mechi ya kwanza katika Dimba la Benjamin Mkapa, Singida Big Stars kukubali kipigo cha mabao 4-1.

Yanga ambao ni mabingwa watetezi wanaongoza ligi hiyo wakiwa na pointi 68 huku Singida Big Stars wakiwa nafasi ya tatu na alama 51.



## SUPA JACKPOT MECHI WIKI HII

### BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 06/05/23 | 17:00 | Wolverhampton Wanderers vs Aston Villa | 2.85 | 3.15 | 2.36 |
| 02. 06/05/23 | 18:00 | OGC Nice vs Stade Rennes | 2.65 | 3.15 | 2.55 |
| 03. 06/05/23 | 19:00 | AS Roma vs Inter Milano | 2.60 | 3.05 | 2.65 |
| 04. 06/05/23 | 21:45 | US Cremonese vs Spezia Calcio | 2.20 | 3.25 | 3.05 |
| 05. 06/05/23 | 22:00 | RC Lens vs Olympique Marseille | 2.23 | 3.40 | 2.90 |
| 06. 07/05/23 | 00:00 | CA Belgrano vs Atletico Tucuman | 2.20 | 2.95 | 2.90 |
| 07. 07/05/23 | 02:30 | Charlotte FC vs New York City FC | 2.41 | 3.05 | 2.55 |
| 08. 07/05/23 | 02:30 | San Jose Earthquakes vs Los Angeles FC | 2.60 | 3.20 | 2.26 |
| 09. 07/05/23 | 02:30 | Inter Miami CF vs Atlanta United FC | 2.36 | 3.15 | 2.50 |
| 10. 07/05/23 | 13:30 | Umraniyespor vs Sivasspor | 2.75 | 3.15 | 2.16 |
| 11. 07/05/23 | 13:30 | Atalanta BC vs Juventus Turin | 2.31 | 3.25 | 2.85 |
| 12. 07/05/23 | 16:00 | FC Nantes vs Strasbourg Alsace | 2.50 | 3.30 | 2.60 |
| 13. 07/05/23 | 16:00 | AJ Auxerre vs Clermont Foot 63 | 2.25 | 3.20 | 3.00 |
| 14. 07/05/23 | 16:00 | FC Lorient vs Stade Brest 29 | 2.22 | 3.40 | 2.90 |
| 15. 07/05/23 | 17:30 | Maritimo Madeira vs Rio Ave FC | 2.43 | 3.00 | 2.90 |
| 16. 07/05/23 | 18:30 | Newcastle United vs Arsenal FC | 2.40 | 3.40 | 2.65 |
| 17. 07/05/23 | 20:00 | Vitoria SC Guimaraes vs FC Vizela | 2.31 | 3.10 | 3.00 |

## MECHI ZA USHINDI


"1" NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA "X" NI TIMU KUTOKA SARE "2" NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

### ALHAMISI - 04/05/2023

| MUDA | GAME ID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 15:00 | 5244 | Vorskla Poltava vs Dynamo Kiev | 3.69 | 3.48 | 1.81 |
| 16:00 | 3288 | Singida BS FC vs Young Africans | 3.69 | 2.81 | 1.80 |
| 16:45 | 2478 | Arman Gohar Sirjan vs Saipa Karadj | 3.06 | 2.80 | 2.40 |
| 16:45 | 4850 | Khalijfars Mahshahr vs Mes Shahr-e Babak | 3.41 | 2.69 | 2.30 |
| 17:00 | 1132 | Chador Malu Yazd vs Esteghlal Khuzestan | 2.80 | 2.59 | 2.80 |
| 17:00 | 1670 | Esteghlal Mollasani vs Shahrdari Astara | 2.10 | 2.81 | 3.74 |
| 17:00 | 2390 | Chooka Talesh FC vs Shams Azar Qazvin | 5.58 | 3.46 | 1.58 |
| 17:00 | 2892 | Shahrdari Hamedan vs Fajr Sepasi | 3.35 | 2.60 | 2.18 |
| 17:00 | 3076 | Backa Topola vs Novi Pazar | 1.60 | 3.61 | 5.06 |
| 17:00 | 4640 | Radnik Surduluca vs Cukaricki St | 5.16 | 3.72 | 1.57 |
| 18:00 | 3667 | NK Dob vs Brinje Grosuplje | 2.62 | 3.13 | 2.45 |
| 18:00 | 4133 | Krka vs NK Ilirija | 1.79 | 3.49 | 3.80 |
| 18:00 | 4557 | US Ben Guerdane vs US Monastir | 2.75 | 2.65 | 2.70 |
| 18:00 | 5191 | Krsko Posavje vs Rudar Velenje | 3.40 | 3.30 | 1.95 |
| 18:00 | 5478 | Jadran Dekani vs NK Nafta | 2.85 | 3.20 | 2.11 |
| 18:30 | 4209 | ASK Bravo vs Tabor Sezana | 1.92 | 3.29 | 3.50 |
| 18:30 | 4264 | Aalborg vs Silkeborg | 2.23 | 3.21 | 2.95 |
| 18:30 | 5571 | Qatar SC vs Al Ahli Doha SC | 1.72 | 3.76 | 3.81 |
| 19:00 | 1394 | Zalgiris Kaunas vs FK Panevezys | 3.30 | 2.85 | 2.06 |
| 19:00 | 1466 | East Riffa vs Manama Club | 5.60 | 3.53 | 1.57 |
| 19:00 | 1805 | AEL Limassol vs Nea Salamis | 2.10 | 3.32 | 3.32 |
| 19:00 | 2333 | AL Badii vs AL Khalidiyah | 7.05 | 5.18 | 1.31 |
| 19:00 | 2720 | Haras EL Hodood vs Talaea El Gaish | 3.67 | 2.81 | 2.19 |
| 19:00 | 4077 | Anorthosis Famagusta vs Olympiakos Nicosia | 1.70 | 3.60 | 4.65 |
| 19:00 | 5623 | Arab Contractors vs National Bank | 2.14 | 2.66 | 4.12 |
| 19:30 | 2857 | Radnicki Nis vs Vojvodina | 3.42 | 3.22 | 2.01 |
| 20:00 | 1993 | IFK Varnamo vs Brommapojkarna | 2.00 | 3.28 | 3.28 |
| 20:00 | 4069 | Norrkoping vs Hammarby | 2.77 | 3.23 | 2.28 |
| 20:00 | 4714 | Varbergs Bois vs Malmo | 5.97 | 4.11 | 1.43 |
| 20:00 | 5011 | IFK Goteborg vs Degerfors | 1.90 | 3.33 | 3.54 |
| 20:30 | 1081 | Copenhagen vs Nordsjalland | 1.68 | 3.73 | 4.25 |
| 20:30 | 1232 | CA Osasuna B vs Numancia | 2.14 | 3.06 | 3.27 |
| 20:30 | 2180 | Basaksehir vs Ankaragucu | 1.95 | 3.31 | 3.52 |
| 20:30 | 2845 | Girona vs Mallorca | 2.10 | 3.10 | 3.45 |
| 20:30 | 4738 | Sevilla FC vs Espanyol | 1.81 | 3.46 | 4.01 |
| 21:00 | 2221 | Al Arabi Doha SC vs Al Gharafa SC | 1.81 | 3.69 | 3.48 |
| 21:00 | 5238 | Lekhwiya SC vs Al Sadd SC | 2.23 | 3.69 | 2.56 |
| 21:15 | 3479 | Maghreb Tetouan vs Olympique Safi | 3.28 | 2.82 | 2.22 |
| 21:15 | 5075 | Luka Koper vs Domzale | 2.03 | 3.24 | 3.24 |
| 21:30 | 1634 | Coca Cola vs Farco FC | 1.74 | 3.22 | 5.03 |
| 21:45 | 3550 | Udinese vs Napoli | 4.13 | 3.46 | 1.79 |
| 21:45 | 4262 | Huddersfield vs Sheffield Utd | 2.95 | 3.05 | 2.37 |
| 21:45 | 5927 | Empoli vs Bologna | 2.85 | 3.05 | 2.43 |
| 22:00 | 5149 | Brighton vs Manchester Utd | 1.96 | 3.66 | 3.26 |
| 22:15 | 3649 | Stjarnan vs Breidablik | 3.47 | 3.79 | 1.83 |
| 22:15 | 3892 | Vikingur Reykjavik vs Keflavik IF | 1.39 | 4.78 | 5.81 |
| 22:30 | 3610 | Porto vs Famalicao | 1.28 | 4.98 | 8.71 |
| 23:00 | 3195 | Athletic Bilbao vs Betis | 1.65 | 3.70 | 4.70 |
| 23:00 | 4021 | Rayo Vallecano vs Valladolid | 1.73 | 3.59 | 4.29 |
| 23:30 | 5263 | Difaa El Jadidi vs Hassania Agadir | 2.77 | 2.98 | 2.42 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

Michezo
Alhamisi Mei 4, 2023
Nipashe



Messi asimamishwa PSG UKURASA 22

‘OOOH YES’!...




Winga wa Chelsea, Noni Madueke, akimzidi ujanja beki wa kati wa Arsenal, Gabriel Magalhaes (kulia) na kuifungia timu yake bao la kufutia machozi wakati ikikubali kipigo cha mabao 3-1 kwenye mechi ya Ligi Kuu England iliyopigwa Uwanja wa Emirates usiku wa kuamkia jana. **PICHA: MTANDAO**

# Nabi awaonya Yanga kwa Marumo Gallants

**Faustine Feliciane na Saada Akida**

●●● Ataja mambo yanayoweza kuwapoteza kwa Mkapa ni wakati wakiivaa Singida BS leo, Pluijm naye asema...

WAKATI wakishuka Uwanja wa Liti mjini Singida leo kuwavaa wenyeji wao, Singida Big Stars kwenye mechi ya Ligi Kuu Bara, Kocha Mkuu wa Yanga, Nasreddine Nabi, amesema wachezaji wake wanapaswa kusahau mafanikio waliyoyapata katika mchezo wa robo fainali Kombe la Shirikisho Afrika dhidi ya Rivers United, ili kuweza kufanya vizuri hatua ya nusu fainali ya michuano hiyo.

**Yanga imefuzu kucheza hatua hiyo baada ya kufanikiwa kuiondosha Klabu ya Rivers United ya Nigeria kwa jumla ya mabao 2-0 iliyoyapata ugenini kabla ya kutoka suluhu katika Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.**

Akizungumza na Nipashe jana, Nabi alisema wanaendelea kuwaandaa wachezaji wao kuweza kufanya vizuri kwenye mchezo wa nusu fainali dhidi ya Marumo Gallants FC ya Afrika Kusini na makosa yoyote watakayoyafanya ndani ya uwanja yatawagharimu.

“Tunafahamu mchezo wetu utakuwa mgumu, wachezaji lazima sasa wasahau mafanikio tuliyoyapata kwenye mchezo wa robo fainali na kujiandaa kuwakabili Marumo, hautakuwa mchezo mwepesi, kosa lolote tutakalolifanya linaweza likatuweka kwenye wakati mgumu “ alisema Nabi.

Aidha, alisema hatua hiyo ya nusu fainali ni ngumu na kila timu iliyofuzu ni ngumu na zimejiandaa kufanya vizuri.

“Tunapaswa kumaliza mchezo hapa nyumbani, matokeo mazuri yatatupa mwanga kuelekea kwenye mchezo wa marudiano ugenini, hatua hii ni lazima tuanze kufanya vizuri kwenye mchezo wa nyumbani,” alisema Nabi.

Yanga itaanza mchakato wa kufuzu hatua ya fainali kwa kuanzia nyumbani mchezo wa nusu fainali Mei 10, mwaka huu utakaopigwa Uwanja wa Benjamin Mkapa kabla ya kurudiana nao wiki moja baadaye nchini Afrika Kusini.

Kuhusu mchezo wao wa Ligi Kuu Bara utakaopigwa leo katika Uwanja wa Liti dhidi ya Singida Big Stars, Kocha Msaidizi wa Yanga, Cedric Kaze, aliiambia Nipashe kuwa wanahitaji pointi tatu katika mechi hiyo kwa lengo la kuendelea kujiweka katika mazingira mazuri ya kutetea ubingwa.

Alisema kila mchezaji anatambua umuhimu wa mchezo huo, na kwa bahati nzuri wote wana afya nzuri yakuweza kupambana.

“Mechi itakuwa ya ushindani mkubwa kwa sababu tunafahamu ubora wa kikosi cha Singida Big Stars na tumejipanga kupata ushindi katika mechi ya kesho (leo).

Hakuna majeruhi na kutakuwa na mabadiliko ya kikosi kidogo kulingana na mazoezi ya leo (jana), lakini pia kutokana na aina ya timu tunayocheza nayo,” alisema Kaze.

Kocha Mkuu wa Singida Big Stars, Hans van Pluijm, alisema amefanya maandalizi mazuri na kikosi chake kipo tayari kwa ajili ya mchezo dhidi ya Yanga kuhakikisha wanapata matokeo chanya.

Alisema licha ya ligi kuwa ukingoni, wanakuwa makini na mechi zote zilizosalia ili kufikia malengo yao na watahakikisha mechi ya leo dhidi ya Yanga wanavuna alama muhimu.

“Tunatambua ubora wa kikosi cha Yanga, kwa sababu wametoka kucheza robo

INAENDELEA UKURASA 23

## Simba yapania kuionesha Azam FC soka la Morocco

**Na Adam Fungamwango**

KLABU ya Simba imesema mpira ambao ulichezwa kwenye mechi ya robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Afrika kati yao naWydad Athletic Club ya Casablanca nchini Morocco, ndio watakaouonyesha kwenye mechi ya nusu fainali ya Kombe la FA dhidi ya Azam FC, hivyo kuwataka wapinzani wao wajiandae kukutana na pumzi ya moto.

Meneja Habari na Mawasiliano wa klabu hiyo, Ahmed Ally, ambaye ndiye aliyetoa kauli hiyo, mbali na hayo amelishukuru Shirikisho la Soka nchini (TFF), kwa kuisogeza mechi yao kutoka Jumamosi mpaka Jumapili wiki hii, uwanja ukiwa ni ule ule wa Nangwanda Sijaona mkoani Mtwara.

Akizungumza kuelekea kwenye mechi hiyo akiwa mkoani Lindi, Ahmed, aliwatahadharisha Azam kukutana na Simba ambayo kwa sasa ipo kwenye kiwango cha juu sana cha soka si la Tanzania, bali barani Afrika.



“Ni mechi ya muhimu sana kwetu, ni ya kutupeleka fainali na kama tutacheza kama tulivyocheza dhidi ya Wydad Casablanca mpaka mashabiki wa timu hiyo wakaufanya uwanja kuwa sehemu ya kufanyia sala, Azam FC anatusumbuaje? Na itakuwa ni maajabu makubwa, unampelekea pumzi ya moto Wydad ya Morocco, halafu anakuja mtu kutoka Chamazi kukusumbua kweli, yatakuwa ni mambo ya kushangaza dunia,” alisema Ahmed.

Alisema kwenye mechi hiyo wanataka waihakikishie dunia kuwa kile ndicho kiwango chao

INAENDELEA UKURASA 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >